

NENO LA MUNGU LINAHITAJI

UTENGANO MKAMILIFU

KUTOKANA NA KUTOKUAMINI



Hebu tuendeleo kusimama, kwa muda mfupi tu, sasa, kwa ajili ya maombi. Na tuinamishe vichwa vyetu. Sijui iwapo, katika kusanyiko letu usiku wa leo, je! kuna yeyote hapa ambaye angetaka kukumbukwa katika maombi? Ifanye haja yako ijulikane tunapoinua mikono yetu kwa Mungu. Vema. A-ha.

Baba yetu wa Mbinguni, tunaukaribia Utakatifu Wako mkuu, usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu, tukiwa na ahadi hii, ya kwamba, “Mkiomba Baba lolote katika Jina Langu,” mtapewa. Tunajua hiyo ni kweli kwa sababu ni Neno Lako. Tupo hapa tukiwaombea watoto Wako wagonjwa, tukijaribu kuona kile tuwezacho kufanya ili kuhamasisha imani. Ninaomba, Baba, kwamba Wewe utatutia moyo kabisa, usiku wa leo. Jalia kila haja iliyojulishwa kwa mikono hiyo. Na labda wengine walikuwa na haja ambao hawakuinua mikono yao, Baba, ninaomba ya kwamba watajaliwa, pia. Jipatie utukufu kutokana na kukutanika kwetu pamoja usiku wa leo, katika Jina lako, tunaomba. Amina.

Mwaweza kuketi.

Nafikiri ni mimi niliye na hatia ya kubadilisha hizi. Lakini daima mimi huogopa kwamba, kupwelewa kwa sauti yangu, sizungumzi kwa sauti kubwa vya kutosha hata nyinyi... Je! mnaweza kunisikia vizuri huko nyuma, sasa? Nyuma kabisa, je! mnaweza kunisikia vizuri? Naam, hilo ni jambo fulani, sivyo? Hiyo ni sawa.

Sasa, tuna furaha sana kuwa hapa tena usiku wa leo, kabla tu ya mkutano huu unaokaribia wa Wafanyabiashara wa Full Gospel. Tunatazamia baraka kubwa kwenye wakati huo. Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atafanya jambo miongoni mwetu, usiku wa leo, ambalo litatuinua sote mawinguni, kama ilivyokuwa, mkutano utakapoanza. Nasi tuna... Mkutano si kuja kwetu pamoja sanasana ili kukutana mmoja na mwenzake, bali sisi—sisi, kuja pamoja katika uwezo wa Roho Mtakatifu. Hilo ndilo huleta mkutano. Tunakuja kukutana na Yeye. Hilo ndilo ku—kusudi letu la awali la kukutanika, ni kukutana na Yeye.

Nina furaha sana usiku wa leo, kuona jukwaani wengi wa marafiki zangu ambao wameanza kukutana: Ndugu Row, na nilikutana na Ndugu King, na Ndugu Brown, hapa, Ndugu Clayton, loo, ni, kila mtu; wote ni rafiki zangu. Na hawa wahudumu wema jijini, hapa, ambao, nimekuwa na ushirika huu pamoja nao kwa miaka mingi na kwa hakika tuna shukrani kwa kila mmoja wao.

Na sasa, sijui tu kwamba ratiba ikoje, bali nina...kwa ajili ya ibada. Tukiwa na wanaume, hapa, kama Ndugu Brown na watu hawa kuhubiri, nina hakika mnaenda kubarikiwa na mahubiri katika wakati wa mkutano. Kwa namna fulani nimetoa nadhiri kwamba badala ya kuwaweka watu kuchelewa sana, ningeweka muda zaidi kuwaombea wagonjwa. Kila mmoja, labda, ambaye amekuwa kwenye mikutano, wanajua aina ya mikutano hii ilivyo, wanajua kile ambacho hufanyika. Kwa hiyo basi, sijisikii kwamba niko miongoni mwa watu wasionifahamu au mtu fulani asiweifahamu ma—maskini namna ya huduma ambayo Bwana amenipa leo hii. Kwa hiyo, ninaenda tu kuufanya ujumbe wangu kuwa rahisi sana kila usiku, na kujaribu kuufanya dakika thelathini, ambapo tumekuwa tukiufanya saa mbili. Kwa hiyo, hilo ni ninii kubwa, tofauti ku—kubwa. Kwa namna fulani ni vigumu unapoanza kwenye wazo fulani, kisha inakubidi kuachana nalo. Bali, kujaribu kuacha ushuhuda mdogo wa mambo yaliyotukia.

Basi kesho usiku kunamaliza ibada zetu tangulizi kabla ya mkutano, kuombea wagonjwa. Jana usiku ilinibidi kuwaacha watu wachache sana ambao sikuweza kuwaombea. Tulikuwa na mstari wa maombi jana jioni, na Bwana akayajibu kwa njia kuu. Mara nyingine. Ninaamini kwamba watu wengi, wengi sana waliponywa, lakini ilinilazimu kuacha wengi wao wakiwa wameshikilia kadi zao, bado. Kwa hiyo niliahidi kwamba ningewaombea usiku wa leo na hilo ndilo ninalokusudia kufanya. Na halafu kesho usiku, mbona, tutawaombea waliobaki, Bwana akipenda. Mnaona.

Sasa, tutafungua katika Maandiko, kwenye Maandiko machache ambayo nimeyaandika hapa, kwa kile mimi (kama ningeikiita fungu, nisingejua kama wanakiita fungu, au la, bali kwa ajili tu ya fungu), ninataka kuchukua wazo hili: *Neno La Mungu Linahitaji Utengano Mkamilifu Kutokana Na Kutokuamini.*

² Na sasa ningependa kusoma kutoka kwenye Biblia, katika Kitabu cha Mwanzo, mlango wa 13 wa Mwanzo, na tungependa kuanzia na kifungu cha 5, kusoma. Ninapenda tu kulisoma Neno. Kwa sababu, nisemacho kinaweza kushindwa, huyo ni mwanadamu. Bali, kama nikisoma tu Neno hili, kile Yeye asemacho hakiwezi kushindwa. Kwa hiyo basi ninajua kutakuwa na uzuri kutoka kwa hilo, kama si zaidi ya kusoma tu Neno. Kifungu cha 5, tunaanza, cha mlango wa 13.

Na Lutu aliyesafiri pamoja na Abram, yeye naye alikuwa na makundi ya ng'ombe na kondoo, na hema.

Na ile nchi haikuwatosha, ili wakae pamoja; maana mali zao zilikuwa nyingi, hata wasiweze kukaa pamoja.

Kukawako...ugomvi kati ya wachunga wanyama wa Abram, na wachunga wanyama wa Lutu; na siku zile Wakanaani na...Waperizi walikuwa wakikaa... katika nchi.

Abram akamwambia Lutu, Basi, usiwepo ugomvi, nakusihi, kati ya mimi na wewe, wala kati ya wachungaji wangu na wachungaji wako; maana sisi tu ndugu.

Je! Nchi hii yote haiko mbele yako? Basi ujitenge nami, nakusihi; ukienda upande wa kushoto, nitakwenda upande wa kuume; ukienda upande wa kuume, nitakwenda upande wa kushoto.

Lutu akainua macho yake, akaliona...bonde lote la Yordani; ya kwamba lote pia lina maji, kabla BWANA hajaharibu Sodoma na Gomora, lilikuwa kama Bustani ya BWANA, kama nchi ya Misri hapo unapokwenda Soari.

Basi Lutu akajichagulia bonde lote la Yordani; Lutu akasafiri kwenda upande wa mashariki; wakatangana...wao kwa wao.

Abram akakaa katika nchi ya Kanaani, na Lutu akakaa katika miji ya lile Bonde; akajongeza hema yake mpaka Sodoma.

Lakini watu wa Sodoma walikuwa wabaya, wenye kufanya dhambi nyingi sana juu ya BWANA.

BWANA akamwambia Ibrahim alipokwisha kutengana na Lutu, Inua sasa macho yako, ukatazame kutoka hapo ulipo...upande wa kaskazini,...kusini,... mashariki,...magharibi;

Maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele.

³ Sasa, wazo, la Neno la Mungu kuhitaji utengano mkamilifu! Tunajua tu hili tunaposoma Neno na kuliona Neno likijidhihirisha Lenyewe.

⁴ Sasa, hapo mwanzo, Mwanzo 1:3, tunapata hilo. "Kulikuwa na giza juu ya nchi. Na Roho wa Mungu alitembea juu ya maji. Kisha kasema, 'Iwe nuru,' na kukawa nuru. Na Mungu akaona kuwa nuru ilikuwa nzuri; ndipo Mungu akatenganisha nuru kutoka kwa giza." Kwa hiyo Neno la Mungu lilianza kutenganisha nuru kutokana na giza, tangu mwanzo, kwa hiyo inabaki hivyo hata wa leo.

⁵ Kama nilivyosema jana usiku, juu ya Yesu, wakati alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili pekee. Na ikiwa ni kosa la mama Yake, ambaye anadaiwa na watu kuwa ni mama wa Mungu, na jinsi ambavyo mwanamke huyo alisema, “Mbona, mimi na baba Yako tumekutafuta kwa machozi.”

⁶ Ndipo upesi Yeye, akiwa ni Neno, kasema, “Hujui kwamba inanipasa kuwa katika shughuli za Baba Yangu?”

⁷ Mnaona, yeye alikuwa akimtangaza kuwa ni mwana wa Yusufu, lakini Yeye hakuwa mwana wa Yusufu. Kama angalikuwa mwana wa Yusufu, angalikuwa pamoja naye; lakini Yeye alikuwa pamoja na Baba, katika shughuli Zake. Kwa hiyo Neno daima husahihisha na daima ni sahihi, nalo Neno litasahihisha kila kosa, daima.

⁸ Sasa wakati dunia ambayo...Mungu alikuwa anaenda kutumia dunia, nayo ilikuwa katika giza totoro. Roho wa Mungu akanena, na kusema, “Iwe nuru,” na Yeye akatenganisha nuru kutoka kwa giza. Na imekuwa ikifanya hivyo tangu wakati huo, kutenganisha Nuru na giza. Neno la Mungu pia lilitenganisha maji na nchi kavu, hapo mwanzo. Mungu alinena, nayo maji yakatenganishwa na nchi kavu. Kwa hiyo, hilo, Yeye alikuwa na sa—sababu ya kufanya hivyo.

⁹ Mungu kamwe haneni Neno isipokuwa awe na sababu ya kulinena Neno hilo. Yeye si kama mimi na wewe, ambao tunaninii tu...ama hasa mimi, ambaye hunena mambo mengi sana ya kipumbavu. Mungu hunena kila Neno likiwa na maana, na jambo fulani analojaribu kutimiza, na atalitimiza kwa Neno Lake. Na Hilo litatenda kile hasa alichosema litatenda.

¹⁰ Sasa, kama Mungu alisema, “Iwe nuru,” na kusiweko nuru, basi hilo—hilo si ninii, hilo si Mungu aliyelisema. Mnaona?

¹¹ Mungu anaposema jambo lolote, Yeye lazima atetee lile asemalo. Na Neno la Mungu likiisha kuthibitishwa, Neno likiisha kuthibitishwa, hilo ni Nuru. Sasa, Neno Lenyewe si Nuru mpaka liwe ni Nuru iliyothibitishwa.

¹² Kama Mungu alisema, “Iwe nuru,” na hakukuwa na nuru yoyote, basi halikuwa ni Neno la Mungu. Bali nuru ilipotokea duniani, hiyo ilionyesha kwamba Neno lilithibitishwa, na ikawa nuru.

¹³ Sasa, leo hii, ikiwa Mungu ametoa ahadi, na wakati ahadi hiyo ikithibitishwa, basi hiyo ni Nuru. Hiyo ndiyo Nuru ya siku hii, wakati Neno limethibitishwa, Neno kwa ajili ya majira hayo limethibitishwa.

¹⁴ Basi, Mungu alikuwa anaenda kuwa na n—nchi ambapo alikuwa anaenda kupanda mimea, na Yeye angekuwa na watu juu ya nchi, ndipo basi akanena na kutenganisha maji na bahari.

Halafu, pia, Yeye alitenganisha, katika Mwanzo, uhai kutoka kwa mauti.

15 Sasa, ikiwa tunaamini Neno la Mungu, Hilo ni Neno la Uzima kwetu; lakini tukiliswali Neno la Mungu, ni kifo kwetu. Kwa kuwa, Mungu amenena, ni nani awezaye kukataa Hilo? Mnaona? Na tukiliswali Neno la Mungu, basi Hilo linakuwa kifo.

16 Kama vile Hawa, sasa, Hawa aliswali sehemu moja ndogo ya Neno la Mungu, na hiyo ikafanya nini? Ikasababisha matatizo haya yote tuliyo nayo. Kama angalidumu nyuma ya Neno, ameimarishwa nyuma ya Neno, silaha zote za Mungu, na asikose kuliadini, basi isingalifanyika jinsi ilivyofanyika, kamwe isingalikuwa hivi ilivyo. Lakini, mnaona, kukaja mauti.

17 Basi, Mungu pia alikuwa na upatanisho. Akiwa na rehema kwetu, Yeye alikubali mauti mbadala kwa ajili ya kifo chao, ambacho wote wawili...

18 Alitenganisha uhai na mauti, pia, katika bustani ya Edeni, na Yeye alifanya hivyo kwa Neno Lake.

19 Pia leo hii anafanya jambo lile lile. Wakati, tuko kwenye giza kuu, kama nilivyozungumzia, Jumapili, giza juu ya nchi, juu ya watu, na giza kuu. Katikati ya haya yote, Yeye angali analinena Neno Lake la Uzima kwa wale wanaotaka kuliadini. Na sasa tunaona kwamba ikiwa...

20 Yesu daima ametuambia kwamba kuna utengano. Nasi tunaona ya kwamba kitu cha mwisho kilichobashiriwa kwa jamii ya wanadamu, kabla ya Siku kuu ya mwisho tutakapopaa kuingia katika Uwepo wa Mungu, kutakuwa na utengano wa mwisho. Yeye atawatenganisha kondoo na mbuzi.

21 Mungu atatenganisha, daima amekuwa akitenganisha, akitengaisha, na hiyo ndiyo anayofanya usiku wa leo. Hiyo ndiyo Yeye hufanya daima. Unaweza kuiona katika kila mkutano. Yeye hutenganisha imani na kutokuamini. Yeye hunena. Hujitangaza Mwenyewe kwa wale watakaomwamini na kuwa na imani katika Yeye.

22 Sasa tunapata ya kwamba, katika Hesabu, mlango wa 6, kwamba wito wa Kinadhiri, wito wa Kinadhiri ulikuwa uwatenganishe na ulimwengu wote, kwa Neno la Mungu. Huo ni wito wa Kinadhiri, kutenganishwa.

23 Tunaona kwamba Samsoni alikuwa Mnadhiri, kwa Bwana, naye alitenganishwa na... kwa alama. Nayo alama hii ilikuwa kwamba ilimpasa kuwa na nywele zake ndefu, zikiwa na vishungi saba. Ilikuwa ni a—alama ya utengano, kwamba aliitwa kwa kusudi.

24 Nami sitaki nianze juu ya hili, kwa sababu nilisema kwamba hilo... nilikuwa tu ninaenda kuzungumza kwa dakika chache.

25 Lakini nafikiri, leo hii, tunapowaona dada zetu wakiwa na nywele ndefu, kama Biblia ilivyosema inawapasa, nafikiri ni alama ya Kinadhiri kwamba wanataka kumfuata Bwana. Na ninajua hilo linasikika lisilovutia, na ni—ni—ninataka hilo

lizame ndani, mnaona, kwa sababu ndivyo lilivyo. Inaonekana kwamba mtu fulani anajaribu ku—kufanya, kutimiza ja—jambo fulani ambalo Mungu aliwaambia wafanye. Haijalishi gharama, ulimwengu unayosema kuhusu Hilo huko nje, ama ni wangapi wanaodhihaki, au wenye kucheka, ama wakosoaji, hayo hayamsumbui mtu aliyetenganishwa kabisa na mambo ya ulimwengu, kwa mambo ya Mungu. Watalitii Neno, na kujitenga na mambo ya ulimwengu, kwa sababu Neno huwatenganisha.

²⁶ Ninajua wanakabiliwa na kukosolewa. Lakini iwapo hatukukosolewa, basi kungekuwa na kasoro fulani. Ulimwengu daima unawajua walio wake. Bali kama nilivyosema, kwamba, kumbukeni, kukosolewa, kwa sababu ya Neno la Mungu, ni utungu tu wa kukua kwa neema Yake. Inaonyesha kwamba umejitenga mwenyewe ili ku—kuwa Mkristo, kutenda kama mmoja, kuishi kama mmoja, kutii kila Amri ya Mungu. Nayo ni—ni nadhiri ya Mnadhiri, kujitenga, wito kutoka kwa Mungu unaokutenganisha na mambo ya Ulimwengu.

²⁷ Ninaamini, usiku wa leo, kwamba kila mwanamume na mwanamke, kila mvulana na msichana, aliyezaliwa na Roho wa Mungu, ni Mnadhiri kwa Bwana; kwa sababu wameyatenga mambo haya, wenyewe, kutoka kwa masumbuko ya ulimwengu na lolote ulimwengu utakalo kusema.

²⁸ Mnaishi katika jiji hili ambapo pana shule mashuhuri. Basi, basi tunaona taifa letu likitoa wito kwa ajili ya kiwango cha juu cha elimu; ambacho ni sawa, siwezi kusema lolote dhidi yake, ila kwamba elimu haiwezi kukupa wokovu. Mwanasayansi anaweza kupasua punje ya ngano na kukuambia ni kemikali ngapi mbalimbali zilizoko ndani yake, bali haiwezi kupata uhai ulioko humo ndani. Elimu inaweza kukusoma, au kukufundisha hisabati, pia—pia inaweza kukufundisha historia na chochote kile, bali haiwezi kukuletea Nuru. Elimu yako haitafanya hiyo.

²⁹ Mungu anayo njia moja ya kukuletea Nuru: hiyo ni pale unapokuwa tayari kujitenga na mambo yote ya ulimwengu, na ma—masumbuko yote ya ulimwengu, na kushikamana tu na Neno la Mungu lililoahidiwa.

³⁰ Paulo alikuwa Mnadhiri kwa Bwana. Alitengwa na kanisa lake la othodoksi, kwa Neno la Mungu aliye hai.

³¹ Haruni alikuwa Mnadhiri kwa Bwana. Alitengwa kutoka kwa ndugu zake, ili kuyabeba mawe ya kuzaliwa na kuwa kuhani mkuu.

³² Ni utengano mkamilifu. Hatupaswi kurudi ulimwenguni tena, au kuwa na uhusiano wowote na ulimwengu, ila kujiambatanisha tu na Mungu. Yesu anakuja kwa ajili ya Bibi-arusi, Mwanamke, Kanisa lililotenganishwa na mambo ya ulimwengu, au shughuli za ulimwengu. Ametengwa na mitindo ya wakati wa kisasa tunaoishi. Ametenganishwa na shu—shughuli na mapokeo ya makanisa. Yeye ametengwa kwa ajili

ya Mungu pekee, naye Mungu ni Neno. Na kama mume na mke walivyo mmoja, vivyo hivyo Bibi-arusi na Neno wanakuwa kitu Kimoja, kwa kuwa Neno linaishi kupitia Bibi-arusi. Hivyo ndivyo. Hizo ndizo sifa zake. Huo ndio utambulisho wake.

³³ Kama ningeweza kutoa P—Ph.D. au LL.D., na kukuonyesha sifa zangu kutoka kwa shirika fulani au kutoka kwa shule fulani, shule hiyo ingetambua sifa hiyo.

³⁴ Lakini sifa pekee aliyo nayo mwaminio ni Neno la Mungu likiishi ndani yake, likionyesha kwamba Yesu Kristo anaishi ndani ya mtu huyo. Huyo ni Mnadhiri aliyetengwa kwa Bwana, aliyetengwa kwa ajili ya Neno. Biblia ilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hukata hata kugawanya, na mafuta ya mfupa, na kuyatambua mawazo ya moyoni.” Hiyo ndiyo sababu Yesu angeweza kuangalia watu na kujua kile walichokuwa wakiwazia; Yeye alikuwa ni Neno.

³⁵ Sasa, Adamu wa kwanza aliyezaliwa duniani, ama, si kuzaliwa, bali kuumbwa na Mungu, Adamu wa kwanza alijitenga kutoka kwa Neno, kuambatana na mke wake. Sasa, angaliweza kukaa na Neno kama angalitaka kufanya hivyo. Bali alijitenga na Neno, ili kuambatana na mke wake.

³⁶ Hivyo hasa ndivyo mshiriki wa kanisa wa kawaida, baridi afanyavyo leo, hujitenga kutoka kwa Neno la kweli lililo hai, ili kushikilia kanisa lao. Ambapo ninii...Hawa aliweka swali juu ya Neno, ikiwa Mungu angeadhibu au la. Shetani aliweka swali; Hawa akaliadini.

³⁷ Ndipo basi wakati kanisa leo hii linaweka swali juu ya Neno, “Je! ni Yeye yule? Je! angali hai katika Kanisa Lake na kufanya ishara Zake na miujiza aliyofanya wakati alipokuwa hapa duniani, ambayo kwa hakika kabisa alituahidi katika Yohana Mtakatifu 14:12?”

³⁸ “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya pia; hata kubwa kuliko hizi atafanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Zitafuatana nao!

³⁹ Swali ni kwamba, kwa watu leo hii, “Je! kweli anamaanisha hivyo?” Halafu unapokubali yale kanisa lisemayo, “Je! kweli anamaanisha hivyo?” ndipo unajiweka katika hali ile ile aliyojiweka Adamu, na kujiunga na mwa—mwanamke wa kanisa la u—ulimwengu huu, na kujitenga kutoka kwa baraka ambazo Mungu amemwahidi kila mwaminio ambaye atajitenga na ulimwengu na kuja kwa Neno. Sasa, hiyo ni Kweli.

⁴⁰ Sisi ni, tumekuwa na majaliwa ya kuishi katika siku ambayo kwamba Neno la Mungu ambalo tumeona limegawanywa kupitia kila wakati, kwa ajili ya mambo fulani kutukia. Basi wakati hili limekusudiwa, wakati mwingine mtu anashangaa jinsi litakavyotendeka. Maprofesa wana wazo lao wenyewe. Bali katika nyakati hizo, Mungu daima amemtuma nabii Wake. Nalo

Neno la Bwana humjia nabii na kuthibitisha Neno kwa ajili ya kizazi hicho. Nao manabii daima walikuwa ni Mnadhiri, aliyetengwa kutokana na kila kitu kingine ili kulitii Neno la Mungu.

⁴¹ Hivi hamkumbuki kile Petro na Yohana walichosema, “Je! yatupasa kumheshimu mwanadamu, ama Mungu?” Wakati walipowaswali kuhusu tukio la Pentekoste.

⁴² Sasa, mtu wa kwanza alijitenga mwenyewe, Adamu wa kwanza, kutoka kwa Neno, kuambatana na mke wake, aliyeswali kama Mungu alitimiza Neno Lake au la.

⁴³ Ni mfano mkamilifu jinsi gani wa mwaminio vuguvugu, mwenye mawazo ya kimwili leo hii, ambaye angali anataka kuambatana na yale mapokeo yao yasemayo, badala ya kuchukua kile Neno lisemacho. Mfano halisi kabisa! Alitengwa, kuambatana na mke wake. Mwaminio wa kimwili ametengwa kutoka kwa Neno, kuambatana na Kanisa.

⁴⁴ Bali wakati Adamu wa Pili alipoubwa, katika tumbo la uzazi la mwanamke, na akaja ulimwenguni, Yeye alikuwa Mnadhiri kwa Neno la Mungu. Alitengwa kutoka kwa ulimwengu, kuambatana na Neno. Sasa, Waebrania, mlango wa 7, kifungu cha 26, inatwambia kwamba, kwamba hao makuhani daima walifariki, lakini huyu Yesu alikuwa mtakatifu na alitengwa kutoka kwa wenye dhambi.

⁴⁵ *Dhambi* ni “kutokuamini.” Hakuna kutokuamini kulikopatikana ndani Yake, mahali popote. Wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, “Ni nani awezaye kunihukumua kwamba nina dhambi?” Dhambi ni “kutokuamini.” “Ikiwa sijatenda yale tu yaliyotabiriwa kwa ajili ya wakati huu, kama sijatimiza matakwa ya kile Masihi anachopaswa kufanya, basi msiniamini.” Kasema, “Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi,” yanawaambia kuwa Yeye ni Nani.

⁴⁶ Kwa sababu, ilikuwa imetabiriwa, tangu Edeni, kwamba kungekuja Mwokozi. Nabii alisema kwamba angezaliwa na bikira, na jinsi ambavyo kwamba angeitwa “Imanueli.”

⁴⁷ Na pia Yeye alikuwa “Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenyezi.” Na hilo ndilo walilomshtakia, kujifanya Mwenyewe Mungu. Yeye alikuwa ni Mungu, na Yeye alikuwa “Mfalme wa Amani, Mungu Mwenyezi, na Baba wa Milele.”

⁴⁸ Hamna Baba mwingine ila Yeye, tukinena kiroho. Yeye ndiye Baba wa pekee, Baba yetu sisi sote. Basi tunaona, waaminio wote, Yeye ndiye Baba yao, wote watakaoliamini Neno Lake. Kwa kuwa, Yeye alitengwa kikamilifu kutoka kwa kanisa, kutoka kwa mapokeo yake, kutoka kwa mama Yake, kutoka kwa ulimwengu, na alifanya lile tu lililompendeza Baba.

49 Sasa, Yeye alikuwa ni mtu tofauti na Adamu. Haijalishi kile mtu yeyote alichouliza; kwake Yeye, Neno, ilikuwa daima ni Neno kwanza. Naye alithibitisha kwamba Neno lilikuwa sahihi.

50 Wakati Shetani alipojaribu kulipaka chokaa Kwake, na kusema, “Imeandikwa...”

51 Yeye alisema, “Naam, na pia imeandikwa...” Alimkabili Shetani, juu ya Neno; kwa kuwa hilo ndilo alilokuwa, Neno.

52 Katika Biblia, Yohana wa kwanza, Mtakatifu Yohana mlango wa kwanza, kasema, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili, akakaa katikati yetu.” Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

53 Daima ni uhusiano na Neno la Mungu lililonenwa, ahadi ya Mungu kwa ajili ya siku hii. Ndipo wakati ikija, ni isiyo ya kawaida sana mpaka ni vigumu kwa watu kuelewa, kwa sababu tumefungwa sana katika—kwa mifumo na mawazo yetu wenyewe, hata ni vigumu kwetu kuelewa iliyo Kweli.

54 Nafikiri wingi wa hiyo ungetumika kwa—kwa Yusufu, katika siku za—za ninii—ninii... za Mariamu, katika uja uzito wake. Yeye, alikuwa anaenda kuwa mama. Naye Yusufu alimpenda, na a—alitaka kuamini. Alikuwa ni mtu mwenye haki, mtu mwema, naye alitaka kuamini hadithi hiyo ambayo Mariamu alikuwa akimsimulia, lakini bado kulikuwa na swali, kwamba, “Sasa, yeye ni mwanamke mwema.” Hapana shaka Mariamu alikuwa amemwelezea kuzuriwa kwake na Gabrieli. Naye alikuwa ni mtu mwenye haki, katika ukoo wa Daudi.

55 Na hata hivyo, huyo mwanamke, ilionekana kana kwamba alikuwa akijaribu kumtumia huyo mwanamume kama kinga, kumwondolea aibu. Kwa sababu, kama aliposwa na huyo mwanamume, halafu akapatikana katika hali hii ilikuwa sawa na uzinzi (Kumbukumbu La Torati inatuambia hivyo), na angepigwa mawe kwa sababu ya tendo hilo. Basi ilionekana kana kwamba alikuwa akimtumia huyo mwanamume kama kinga.

56 Naye mwanamume yule, mtu mwema, mtu mwenye haki, Biblia ilisema alikuwa ni mtu mwenye haki. Lakini tukio la mwanamke huyu lilikuwa lisilo la kawaida asingeweza kulielewa. Angeweza kuangalia uso wake wa kupendeza, na unyofu na uaminifu ambao angeusimulia hadithi yake. Na hapana shaka ila angeenda nyumbani kwake, ama kwenye karakana yake ya seremala, aseme, “Si—siwezi kuona jinsi angeweza kunidanganya, lakini kisa hiki si cha kawaida kabisa.”

57 Iwapo angalichunguza tu Maandiko, kwamba, “bikira atachukua mimba”! Mnaona, ilikuwa si ya kawaida kabisa kwake, kwa sababu ilikuwa nje ya mwelekeo wa mawazo yake, bali yeye alikuwa kabisa katika Maandiko.

58 Na ndivyo ilivyo leo hii, ndugu, kwamba nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo na Neno Lake lililoahidiwa la wakati huu ni lisilo la kawaida sana, watu wazuri wanakwazika juu Yake. Si la kawaida kabisa. Wanasema wa—wafu walifufuka, vipofu wanaona, viziwi wanasikia, Roho Mtakatifu anatambua mawazo, anabashiri mambo yanayotimia, hayajashindwa hata wakati mmoja. Loo, wao—wao hawawezi, hawawezi kulielewa. Ni lisilo kawaida kabisa, kwa hiyo wao—wao wanasema, “Vema, ni kuwasiliana kimawazo, au ni pepo mwovu,” kama tu walivyofanya siku ile. Kutokuwa kawaida kwa Neno la Mungu!

59 Lakini mtu anapozaliwa ulimwenguni, kama mwa—mwaminio, anakuwa Mnadhiri wakati akijitenga kutoka kwa chochote kilicho kinyume na Neno. Utengano mkamilifu! Yesu alisema, “Nilikuja kumtenganisha mtu na mke wake, kuivunja familia. Na yeye ambaye hatachukua msalaba wake, na kunifuata, hastahili kuitwa Wangu.” Utengano, kutoka kwa kila kitu, chochote; kutoka kwa kanisa, kutoka—kutoka kwa jamii, kutoka kwa imani fulani, ama kutoka kwa familia, au chochote ambacho kingeweza kusimama kati yako na kuamini Neno lote la Mungu. Ikiwa nafsi yako haitaitikia kila ahadi ya wakati huu, kwa “amina,” kuna kasoro mahali fulani. Unahitaji kutenganishwa.

60 Kwa hiyo Yesu alikuwa ni Neno lililofanyika mwili, na Yeye alitengwa kabisa kutoka kwa wenye dhambi, wasioamini, hata Neno Lenyewe likabubujika kikamilifu, na—na likapaa kabisa kupitia Yeye, hata akasema, “Sifanyi lolote mpaka nimwone Baba akilitenda kwanza.” Walikuwa wanauliza, wakimswali kuhusu mambo. Akasema, “Amin, nawaambia, Mwana hatendi neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda.” Basi, tazama, kila kitu alichosema kilikuwa kikamilifu. Ninii tu, haikumbidi kuuliza kukihusu, kuwazia kukihusu; kilikuwa kikamilifu. Nayo Kweli Yake kamilifu daima ilitenganisha Kweli kutoka kwa makosa.

61 Hata vile nitakavyorudia kunukuu tena, tena, mama Yake alisema, “Mimi na baba Yako,” mbele ya wale makuhani ambao alikuwa ameshuhudia alikuwa ni Mwana aliyezaliwa na bikira. Bali katika nyakati zake za huzuni. . .

62 Mvulana wa umri wa miaka kumi na miwili angewezaje, wala hatuna taarifa Yake hata kuenda shuleni, akili Yake ingewezaje kuwa nyingi hata kubishana na makuhani, wenye hekima, watu wenye elimu? Na mbona, wakati, alipomwita huyu Yusufu kuwa ni baba Yake, upesi Neno la Mungu. . . Yeye alitenganishwa. Alikuwa ni Neno, nalo Neno likasahihisha kosa, “Hamjui kwamba inanipasa kuwa katika shughuli za Baba Yangu?” Huyu hakuwa tu ni yule mvulana mdogo wa miaka kumi na miwili. Huyu alikuwa ni Neno la Mungu akinena kupitia maskini kinywa Chake cha kitoto, kusahihisha kosa;

akitenganisha, kama alivyofanya hapo mwanzo, giza kutoka kwa nuru, uongo kutoka kwa Ukweli, mauti kutoka kwa Uzima.

⁶³ Ni kutenganishwa. Daima Neno huhitaji utengano kamili na mtimilivu, haidhuru. Yesu alisema, “Hebu neno la kila mtu liwe uongo; acha Langu liwe kweli.”

⁶⁴ Kote katika nyakati, jambo lili hili limetendeka. Ni kutenganishwa. Daima Yeye huwatenga watu Wake kutoka kwa kutokuamini. Alifanya hivyo wakati wa mwanzo; anafanya vivyo hivyo leo hii. Kila mmoja wa manabii alitengwa na kutokuamini. Wao, sababu yao kufanya hivyo, ni kwa kuwa Neno la Bwana liliwajia.

⁶⁵ Sasa, ninaamini katika usiku mmoja, mahali fulani, labda ilikuwa hapa Jumapili ama jana usiku, ambapo nilikuwa nikizungumzia kile ambacho neno “mwonaji,” katika Agano la Kale, lilimaanisha. Lilimaanisha mtu, “mtabiri, mtu ambaye angebashiri matukio ya baadaye yaliyokuwa yanakuja kutimia.” Ndipo basi yalipotimia sawasawa, bila kukosea, yakatimia hasa kama alivyosema, basi Mungu alisema, “Msikieni mtu huyu, ama msikieni, mwgopeni, kwa kuwa niko pamoja naye.” Basi alikuwa na tafsiri ya Kiungu ya Neno lililoandikwa, kwa kuwa hiyo ilikuwa ni sifa yake ya utambulisho, kwamba alikuwa ni nabii wa Mungu nalo Neno lilimjia. Hiyo ni kweli.

⁶⁶ Sasa, utengano. Ilimtenganisha Isaya kutoka kwa ulimwengu wa kanisa. Ilimtenganisha Musa kutoka kwa ulimwengu wa kanisa. Iliwatenganisha kina...manabii wote mashuhuri, kote katika nyakati, kutoka kwa ulimwengu wa kanisa. Kwa sababu walikuwa na...Ilimtenganisha Yesu kutoka kwa ndugu Zake. Iliwatenganisha mitume kutoka kwa kanisa lililokuwako siku hiyo, Mafarisayo, Masadukayo, watu mashuhuri, watu watakatifu, watu wema, watu wazuri, watu wanyenyekevu, watu waliokuwa na tunda la Roho zaidi sana ya yale Yesu aliyoonyesha.

⁶⁷ Lakini utambulisho Wake ulikuwa ni nini? Kwamba Neno lilikuwa pamoja Naye, Neno lililoahidiwa la siku hiyo lilikuwa linaishi kupitia Yeye. Alisema, “Ni nani kati yenu awezaye kunihukumu kuwa nina dhambi? Ni nani kati yenu awezaye kusema kuwa yale niliyosema hayajatukia?” Hilo, kwa sababu alionyesha kwamba Yeye alikuwa ni Mnadhiri wa Bwana aliyetengwa. Alikuwa ni Bwana Mwenyewe katika mwili.

⁶⁸ Ibrahimu, pia, alikuwa ni mtu aliyetengwa, kutoka kwa ulimwengu, wakati Mungu alipomwita Ibrahimu kwenye umri wa miaka sabini na tano. “Jitenge mwenyewe kutoka kwa jamaa zako na kutoka kwa kutokuamini kote, na uje katika Ulimwengu ambao hujawahi kutembelea hapo kabla, na miongoni mwa watu ambao hujawajua hapo kabla. Toka na ujitenge na mtu yeyote ambaye atakuwa kinyume na yale unayoamini, ili uwe Mnadhiri

kwa Bwana.” Kwa sababu, alikuwa anashikilia ahadi ya mwana. Ilimbidi kujitenga na baba yake, na mama yake, na jamaa zake.

⁶⁹ Basi ni kitu gani kilichomtenganisha? Si kwa sababu kwamba alikuwa ni mtu mwema, bali kwa sababu aliamini kwamba Mungu aliweza kutimiza ahadi aliyokuwa amempa.

⁷⁰ Ndipo wakati alipokuwa miaka ishirini na mitano baadaye, naye mtoto alikuwa hajaja bado; Sara akiwa na miaka tisini, naye mia moja. Ndipo wakati Malaika wa Bwana alipomtembelea; ambalo Yesu alirejelea, kwamba lingejirudia tena katika siku za mwisho. Mungu, katika umbo la kibinadamu, aliketi chini mbele zake na kuzungumza. Naye Sara, akiwa na umri wa karibu miaka mia moja, katika hema nyuma Yake, alicheka kwa sababu Malaika alisema, “Nitakuzuru kulingana na wakati wa ahadi.”

⁷¹ Naye akasema, “Mimi nikiwa mkongwe, na niwe na raha tena na bwana wangu, huku yeye ni mkongwe?”

⁷² Basi Mtu huyu, ambaye alikuwa ni Mungu katika mwili, akasema, “Kwa nini Sara akacheka, ndani ya hema?” Sasa, alitoka nje mbio na kujaribu kulikana. Lakini Yeye akasema, “Naam, bali ulicheka,” kwa sababu kwamba hakuamini hilo lingeweza kuwa sahihi.

⁷³ Sasa, angalieni, Yesu alisema hilo lingejirudia tena. “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Kwa mara nyingine Roho wa Mungu atakuja juu ya mwili, wanadamu wapatikanao na mauti. Mtu huyo alikula nyama ya ndama, akanywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, na kula siagi na mkate, katika mwili wa kibinadamu; naye Ibrahimu alisema Huyo alikuwa Elohimu, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Yesu aliahidi kwamba Mungu, kabla ya kuja Kwake, angedhihirishwa katika mwili wa kibinadamu tena. Huyo ni Roho Mtakatifu (kuna Mungu mmoja tu) akijidhihirisha Mwenyewe, akitenganisha, tena, Lutu na Ibrahimu.

⁷⁴ Lutu alitaka ulimwengu. Mungu alite... aliurua ulimwengu wake, na kumtenga Ibrahimu na Lutu. Lutu, akiwa ni mfano, tena, wa mwaminio wa kimwili ambaye hakudhania mambo haya ni kweli, yeye alienda tu huko chini Sodoma. Na yeye—yeye hakuwa na ujasiri halisi wa kusimama, jinsi tungeuita, na kutaja kuwa “sahihi” kilicho sahihi, na kosa kilicho “kosa,” kwa hiyo akaenda huko chini.

⁷⁵ Hawa waaminio wote, kama vile tungeendelea kwa saa nyingi, hawa wote walikuwa ni kama lundo la chenji kutoka kwa mfuko wako, katika mikono ya Mungu. Unatoa lundo la chenji. Kuna mapeni, vijisenti, mashilingi, robo, nusu dola, dola, zote zikiwa ni sarafu. Sasa, hivyo ndivyo ulimwengu ulivyo, katika mkono wa Mungu. Kuna watu wengine ambao wanaweza tu kuwa na thamani yake ya peni moja, na Mungu anaweza

tu kuwatumia kwa njia ya peni. Hayo tu ndiyo wanayoweza kununua. Usiwakatae. Ikiwa hawawezi kuamini Kweli halisi, usiwakatae, usiwatupe nje na kusema hawako ndani ya Hilo, kwa sababu Mungu hutumia mapeni wakati mwingine.

⁷⁶ Lutu alikuwa ni peni tu, Ibrahimu alikuwa ni dola ya fedha, kwa hiyo ilihitaji Lutu mia moja kufanya Ibrahimu mmoja. Na vivyo hivyo inahitaji... Waaminio mia moja wa kimwili hawatasimama uweponi mwa Mkristo halisi aliyetenganishwa na mambo ya kimwili ya ulimwenguni, anayeishi ndani ya Kristo Yesu, ambapo Neno linaweza kufanya kazi kupitia yeye.

⁷⁷ Anaweza tu kuchukua thamani ya peni moja; hiyo ndiyo tu aliyonayo. Kwa hiyo unawaona watu wanaosema, "Siamini katika uponyaji. Siamini mambo haya," jua tu kwamba ni peni moja, lakini uachane tu naye. Mnaona? Thamani ya peni moja tu, na kwa hiyo hayo tu ndiyo awezayo kununua. Usimzuie; achana tu naye. Kumbukeni, huo tu ndio umbali awezao kufikia.

Yusufu, alitenganishwa na ndugu zake.

⁷⁸ Naam, kamwe sikumaanisha hiyo katika njia hiyo niliyoisema, unaona. Ninamaanisha, kama yeye tu ni, "Vema, mimi ni mfuasi wa hili, na hilo ndilo tunaloamini." Ni peni moja tu, endelea, unaona; peni moja tu.

Unasema, "Vema, Bwana akubariki, ndugu yangu."

⁷⁹ Unaona, huyo ni shaba nyekundu; hawezi kuwa fedha. Jambo ndilo hilo, kwa hiyo liache tu liendele. Mungu anaweza kumtumia. Loo, Yeye anaitumia. Afadhali nimwone huko chini kanisani kuliko kuiona baa imesimama pale pembeni. Si ungetaka iwe hivyo? Hakika. Kwa hiyo achana tu nayo. Mungu anaweza kuitumia, hata hivyo; labda si sana, bali Yeye atatumia kile anachoweza kutumia, kadiri watakavyomruhusu atumie.

⁸⁰ Kwa hiyo kwa namna fulani hiyo ni njia fidhuli ya kueleza chochote, bali mimi... Vema, natumai mnaipata Kweli ninayomaanisha katika hilo, kile—kile linachomaanisha. Mnaona?

⁸¹ Hawezi kuamini katika utambuzi na nguvu za Mungu zilizoahidiwa kwa ajili ya siku hii.

⁸² Wale Mafarisayo wasingeweza kuamini, pia. Wasingeweza kumwona Yesu kuwa ni Mungu. Loo, la. "Unajifanya mwenyewe kuwa Mungu; mwanadamu?"

⁸³ Siku moja alikuwa amesimama pale, baada ya kuzidisha boflo za mkate, na kadhalika, kwa ajili yao, ndipo akasema, "Msipoula m—mkate wa mwili wa Mwana wa Adamu, na kunywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu."

⁸⁴ Loo, ninawazia, kusanyiko Lake, waliondoka wakamwacha. "Mtu huyu anatarajia kuwa sisi ni wala watu, kula mwili wa mtu? Loo, huo ni wazimu!" Madaktari na madaktari wa tiba, na kadhalika, walisema, "Mtu huyu ni mwendawazimu. Hayo

tu. Kuhani yuko sahihi. Mtu huyo ni wazimu. Ati atupe mwili wake tule?"

⁸⁵ Hayo tu ndiyo aliyosema, mnaona, lakini nia ya kiroho, labda hawakuweza kuelewa Hilo. Wale wanafunzi, hawakujua hasa kile Hilo lilichomaanisha, bali waliliamini hata hivyo. Kwa sababu, Hilo lilitoka wapi? Lilitoka kwa Yule waliyemjua kuwa ni Mwana wa Mungu.

⁸⁶ Huenda nisiweze kuelewa yote yaliyoko hapa ndani, bali ninaiamini. Ni Neno la Mungu. Ninataka kujitenganisha mwenyewe kutokana na chochote kilicho kinyume cha Hiyo. Nimejaribu kusimama namna hiyo.

⁸⁷ Tazama kundi jingine, wale sabini, aliowaita. Siku moja Yeye alikuwa amesimama, akizungumza nao, ndipo akasema, "Mwana wa Adamu atapaa kwenda Mbinguni kule alikotoka."

⁸⁸ Wakasema, "Mtu huyu? Ametupeleka mahali alipozaliwa. Tunamjua mama yake, Mariamu. Mbona, tunawajua ndugu zake. Tunawajua wote. Halafu basi Mtu huyu anaenda kuchukua... Mwana wa Adamu anakuja, anapaa kwenda juu Mbinguni kule alikotoka? Alitoka Bethlehemu. Alifanyaje hilo?" Mnaona, Yeye aliisema kwa njia hiyo, mnaona, nao hawakutembea Naye tena. Waliondoka wakaenda. Wakasema, "Aa, Mtu huyu, tunajua ana kasoro fulani."

⁸⁹ Hao wanafunzi wakakaa pale pale. Mnaona? Waliamini. Walikuwa wameliona Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo, likithibitishwa na kudhihirishwa na Yeye. Ni nani aliyeweza kuumba, isipokuwa Mungu Mwenyewe, angeweza kuchukua mkate na... Walijua Huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu. Kama ilikuwa katika mafumbo au la, kwamba walielewa Hilo au sivyo, waliendelea na safari, kwa vyovyote vile, kwa sababu Neno lilithibitishwa, nao walitenganishwa na chochote kinyume na Hilo.

⁹⁰ Mungu atusaidie kuwa na imani kama hiyo! Tunaiamini Biblia hii kuwa ni Kweli. Huenda nisiwe na imani ya kutosha kuzifanya ahadi zote kutimia, bali ninaamini Hiyo, kwa vyovyote vile. Ninaamini saa hii tunayoishi.

⁹¹ Yusufu, alitenganishwa na ndugu zake, bila sababu. Sasa, shida yao ilikuwa ni nini? Hakuwa tayari kutenganishwa; hayakuwa ni mapenzi yake kutengwa. Bali walijitenga wenyewe kutoka kwake, unaona, kutoka kwa dola yake angavu, inayong'aa; thamani yao ya peni isingestahimili hiyo. Walijua walikuwa ni wazee. Walijua kwamba Isaka alikuwa nanii wao... ama, samahani, Yakobo alikuwa ni baba yao. Nao walijua hiyo kuwa ni kweli. Lakini Yusufu alizaliwa... Asingesaidia hiyo. Alikuwa ni wa kiroho. Aliona maono, aliweza kutafsiri ndoto, na zilikuwa kamilifu kabisa. Lolote alilosema, lilikuwa ni kweli. Nao ndugu zake wazee, walisogea kwa wivu, wakamwiza kwa Wamisri. Mnaona, wao—walijitenganisha

wenyewe naye kwa sababu walikuwa mapeni. Yeye alikuwa ni wa thamani tofauti.

⁹² Ndivyo ilivyo na mwaminio halisi leo hii, yeye ni wa thamani tofauti. Watajitenganisha, (hawaelewi Hilo), shaba nyekundu kutoka kwa fedha.

⁹³ Sasa tunaona, walienda na wivu wakamwiza. Kwa nini? Wanafanya jambo lile lile leo hii. Kilichokuwa hasa, walisema walikuwa... Ilitokana na wivu. Hawakutaka kuvunjika, kwa sababu kwamba thamani iliyokuwa ndani yao haikuwa ndiyo thamani iliyokuwa ndani yake. Basi, kwa sababu ya hiyo, walikuwa na wivu, kwa sababu wao walikuwa mapeni naye alikuwa ni dola. Mnaona?

⁹⁴ Sasa, iwapo peni ingesema, “Jina la Bwana libarikiwe! Ndugu yangu, dola hapa, unaona, siwezi kufanya chenji afanyayo yeye, bali nitafanya kile niwezacho.” Hivyo ndivyo, tungeendelea basi. Mungu angemaliza mpango Wake ipasavyo.

⁹⁵ Kama nilivyowahubirieni, Jumapili, mdundo mkubwa wa Neno la Mungu ukipigwa. Mabadiliko na njia panda ni Mungu tu akibadilisha nyakati, kama vile ki—kiongozi katika mdundo. Tunapoona mabadiliko haya ya nyakati na mabadiliko ya majira, angalia chini kwenye Karatasi *hapa*, nawe utaona tunapaswa kuwa hapa. Inawapasa kutenda hili; hakuna njia kwao kulikwepa.

⁹⁶ Nao muziki, kwa mtu asiyelewa mdundo, ni kitu gani? Ni lundo la kelele za kutatarika. Hauaelewi. Hata haumvutii. Anatamani, “Laiti wangelifunga, ili niweze kwenda nyumbani.” Haumvutii, maana hajui huo mdundo. Haujui.

⁹⁷ Bali Mtunzi anajua mwisho tangu mwanzo. Unaona? Na iwapo kiongozi hayuko katika Roho yule yule wa Mtunzi, hawezi kuutekeleza, kwa kuwa wote unafanywa kwa ishara. Na ikiwa ishara haithibitishi Huo, wanamuziki watachezaje Huo? Amina! Jambo ndilo hilo.

⁹⁸ Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani awezaye—awezaye, ni nani atakayejua jinsi ya kujitayarisha kwa vita, kurudi nyuma, ama chochote cha kufanya?

⁹⁹ Litazame Neno na uone mahali tunapoishi, ndipo unaweza kuona mapeni, kile yafanyacho. Lakini unaweza kuwaona wale wanaong’aa, wanaotazamia, na wanajua Neno, na kutazamia ishara hizi kutukia. [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] Hilo hapo.

¹⁰⁰ Kama vile maskini mwanamke yule pale kisimani, wakati Yeye aliposema, “Nenda kamwite mumeo,” akasema, “Sina mume.” Kasema, “Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano.”

¹⁰¹ Mwanamke huyo akasema, “Bwana, natambua kwamba wewe ni nabii. Hatujakuwa nao kwa mamia ya miaka. Bali

tunajua Masihi yuaja, na Yeye atakuwa ni nabii. Hilo ndilo atakalofanya.”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

¹⁰² Loo, mdundo wa muziki ulienda tu sawa kabisa, kutoka kwa sauti ya chini hadi ya juu. Akakimbia kwenda mjini, akasema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini kuwa huyu ndiye Masihi yeye yule tuliyekuwa tukimtazamia?” Hakika.

¹⁰³ Mnaona, yeye alielewa kile karatasi ya Muziki ilichokuwa katika mdundo, ule unaotenganisha imani na kutokuamini. Imani inaweza tu. . . Si kuja kwa kanisa; imani huja kwa kusikia Neno la Mungu, kujua kwamba Hilo ni kitu gani. Sasa tunaona jambo lile lile leo hii.

¹⁰⁴ Watu wengi huangalia karama. (Katika kufunga sasa, dakika zingine tano.) Watu huangalia karama, ndipo wanawazia, “Loo, kitu kikuu jinsi gani,” nao wanajaribu kuiga karama. Huwezi kufanya hivyo. Unanini tu. . . Huwezi kuifanya pe—pe—peni kuwa dola, huwezi kuifanya kuwa shillingi, unaona, huwezi kuifanya ndururu. Ni peni. Lakini ikiwa tu utajitambua kuwa ni peni, na uambatane na chenji zingine, unaona, Mungu anaweza kukutumia. Huenda tusiweze kufanya yote. Hakukuwa na kila mtu. . .

¹⁰⁵ Wakati Mungu alipowaita Israeli kutoka Misri, haikumbidi kila mmoja wao kufanya jambo lile lile alilofanya Musa, bali waliliamini. Hiyo ni kweli. Walimwamini Musa, kwa sababu walijua kwamba ilikuwa ni ishara ya majira hayo, na kwamba Mungu alikuwa amethibitisha kwamba alikuwa na Neno Lake.

Wakasema, “Farao anayo mikuki.”

Akasema, “Lakini Musa analo Neno Lake.”

¹⁰⁶ Jambo ndilo hilo. Kina Farao huenda wana jeshi, bali Musa alikuwa na Neno kwa sababu alikuwa ni nabii wa Mungu. Nalo Neno lilimjia, na lilikuwa limethibitishwa kwamba Hilo lilikuwa ni Kweli. Ilikuwa ni Mungu aliye hai Yule aliyeweza kuchukua mavumbi na kuyarusha juu na kufanya nzi kutokea. Mwanadamu hawezi kufanya hilo. Kama mtu aliyesimama pale, na kusema, “Kesho yapata wakati kama huu kutakuwa na *ninii na ninii*,” na ikawa. Mnaona? Walijua Musa alikuwa na Neno la Mungu. Haijalishi ni mikuki mingapi na magereza aliyokuwa nayo Farao, na ni motafali ngapi za kutengeneza; Musa alikuwa na Neno, kwa hiyo wakaanza safari kwenda nyikani.

¹⁰⁷ Kulikuwako na mtu, Dathani, kasema, “Musa anajitwalia mengi kupita kiasi. Sisi sote ni watu watakatifu, kwa hiyo sote tunapaswa kuwa na uwezo kufanya yale aliyofanya Musa.”

Ndipo Musa akasema, “Mungu, vipi kuhusu hili?”

¹⁰⁸ Akasema, “Jitenge. Kaa mbali nao.” Ndipo akaifungua nchi, na kuwameza Dathani na kundi lake.

109 Alitenganisha Nuru na giza, kwa kuthibitisha Neno Lake. Yeye ni Mungu yule yule leo hii.

110 Ninafunga. Nilikuwa nikiwaambieni, jana usiku, nilipokuja hapa kwa mara ya kwanza. Hili si la kibinafsi. Kama unawazia hivyo, basi tafadhali yavute tu mapazia kwa moyo wako. Ninasema haya kwa wale wanaoamini.

111 Ilinenwa na kutaja hasa yale mambo ambayo yangetukia, kote katika wakati, nanyi nyote ni mashahidi wa jambo hilo, kama mlivyoshuhudia jana usiku, kutokana na utambuzi, kuendelea. Na jinsi ambavyo kungekuwa na waigaji, miigo, na kila kitu kikitukia.

112 Bali, jambo la mwisho, kulikuwa kuwe na jambo kuu likitendeka. Tume kuwa tukilitazamia kwa miaka. Nasi sote tunajua wakati lilipotendeka mara ya kwanza, wakati umbaji ulipotokea, mara ya tatu. Na halafu mara ya nne. Jana usiku niliwaambia mara ya tano ulipotukia.

113 Nao unangojea hili Baraza la Makanisa, wakati likiungana, na Waprotestanti. Kama nikinena Jumapili asubuhi, hilo ndilo ninalotaka... Ninamaanisha Jumamosi asubuhi, hilo ndilo ninalotaka kuzungumzia, mnaona, sasa. Ndipo basi hili likiunganika pamoja, basi Roho wa Mungu daima huihua kiwango dhidi yao. Mnaona?

Yupo mtu anayeketi hapa, usiku wa leo, ambaye ni shahidi wa jambo hili.

114 Nilikuwa huko Colorado, si muda mrefu uliopita, majira haya yaliyopita ya kupukutika. Mimi huenda huko kwa ziara za kuwinda. Na, kama kawaida, mimi huwa huko juu kwenye ukumbusho wa kila mwaka wa ndoa yangu. Wakati tulipooana na mke wangu, ni—nilikuwa nimeweka akiba vijisenti vyangu na kadhalika, na kutokana na kazi yangu, na niliziweka katika mkebe wa hamira. Nami sikuwa na za kutosha kugharamia fungate, na kwenda kuwinda; kwa hiyo nikaweka tu zote mbili pamoja, na nikampeleka kwenye ziara ya kuwinda, kwa ajili ya fungate. Kwa hiyo tangu wakati huo, nimekuwa, kwa aibu yangu, sijawahi kuwa nyumbani pamoja naye kwenye ukumbusho wetu wa kila mwaka. Nilikuwa Colorado.

115 Jana usiku niliwaona wahudumu wawili au watatu walikuwa hapa, waliokuwa pamoja nami huko juu kwenye kambi, mahali ilinibidi kushuka kutoka Alaska na kukutana nao, kuwinda. Ilikuwa ni wavulana wa Martin. Walikuwa hapa jana usiku. Mimi... Wapo hapa, huko nyuma kabisa. Halafu maskini jamaa yule mwingine, ninasahau jina lake, anayeketi... Je! ulikuwepo, pia, mwanangu? Hiyo ni kweli. Na labda je! Ndugu Palmer yupo hapa? Mimi... Na tulikuwa huko juu milimani. Nami ni kiongozi huko Colorado, nimewinda humo ndani kwa miaka.

¹¹⁶ Basi kila wakati ukumbusho wetu wa kila mwaka, tarehe ishirini na tatu Oktoba, huja... Kuna mahali padogo ambapo nilimpeleka mke wangu kwenye fungate yetu, juu kwenye Milima ya Adirondack, na mahali hapa huonekana tu kama pale, ila tu pale palikuwa... Hapa ni miti mitetemo hapa juu, kichaka kidogo, na kule juu kulikuwa mti wa Ulaya. Nami hutembea huko nje, tarehe ishirini na tatu, wakati fulani katika mchana, ninavua kofia yangu na kumshukuru Bwana kwa ajili ya mke mwema, mtiifu ambaye amekuwa mtiifu na mwema kwangu kupitia miaka hii, na amenisaidia, wakati ninapoenda kuhubiri Injili.

¹¹⁷ Na kumekuwa kukavu sana huko Colorado mwaka huu, kama ambavyo imekuwa kote nchini. Ndipo mara moja kukawa... Nadhani kulikuwa na watu mia mbili wametutangulia, ama watu mia moja, samahani, yapata watu mia moja mbele yetu, huko juu ya makambi. Nao walikuwa wakipiga risasi huko juu, kwa siku nne ama tano. Nami nilikuwa nimempiga risasi kulungu, yule niliyekuwa nikimwinda kwa miaka. Pia, bali mimi... kukaja ukungu, nami sikuweza kumwona; nisingeweza kumpata. Nami nilikuwa nikimsaka siku hiyo.

¹¹⁸ Basi siku iliyofuata, simu ama ninii... ikaja kwenye redio, "Dhoruba inakuja, huenda ikamimina futi ishirini ya theluji katika milima hii usiku kucha."

¹¹⁹ Basi kwa hiyo nikawaambia ndugu. Niliwaita ndani. Wavulana wa Martin walikuwapo pia. Nikasema, "Ndugu, mmesikia kile habari imesema. Sasa, ikiwa mnataka kuondoka, afadhali mwende sasa hivi, maana itakuwa imechelewa sana. Huenda mkakaa hapa kwa juma moja. Nami ninapaswa kuenda, kwa sababu Jumatatu ijayo nina mkutano, wafanyabiashara Wakristo, Wafanyabiashara wa Full Gospel kwenye tawi huko Tucson. Hata hivyo, jiamulieni wenyewe. Mkitaka kubaki, mimi ni kiongozi wenu, nitakaa hapa pamoja nanyi."

Kila mmoja wao akapiga kura, "Tutakaa. Tutakaa."

¹²⁰ Wale wavulana wa Martin, wakiwa na gari lenye mwendo wa polepole, ama gari lenye mwendo wa kasi, hasa, wote... Tulikuwa na kulungu kadhaa wa zaidi kule, tukawapa wavulana wa Martin na wengine, nao wakaondoka; maana wasingetoka kule, hivyo tu. Kwa hiyo, wao, wameketi hapa kama shahidi usiku wa leo.

¹²¹ Halafu siku iliyofuata, niliwazia... Vema, hakukuwa na theluji siku hiyo, siku ile waliyotoka. Nikasema, "Nitampigia mke wangu simu na kumwambia ninashukuru kwa kuwa amekuwa ni mke mwema, na kadhalika. Ni ukumbusho wake wa kila mwaka. Ndipo kesho nitaenda mahali pale, tukifika kule juu, kwa sababu ya theluji."

¹²² Na kwa hiyo ni—nikaingia ndani, na nisingeweza kumpigia simu. Nikarudi. Na kila mtu mjini akijitayarisha, nayo dhoruba kubwa ilikuwa inakuja, nalo gazeti lilisema “ingeweza kumimina futi ishirini ya theluji katika Colorado,” usiku huo.

¹²³ Ndugu Tom Simpson yupo ameketi hapa mahali fulani usiku wa leo, ama anapaswa kuwa. Yeye alikuwa huko Canada na alikuwa njiani akiteremka, nao wakapita kando. Kasema, “Kwepa Colorado! Dhoruba kuu!” Je! upo hapa, Ndugu Simpson? Uko wapi? Naam, ameketi nyuma hapa nyuma. Nao walimwambia, “Kwepa Colorado. Dhoruba kuu inakuja.”

¹²⁴ Kwa hiyo ni—nikamwambia dada, na—na mke wa mtu mwingine, wa Ndugu Evans. Sidhani Ndugu Evans yupo hapa usiku wa leo, isipokuwa ameingia tu sasa hivi. Je! upo hapa, Ndugu Evans? Na sidhani amefika hapa bado. Atakuwa hapa kwenye mkutano, hata hivyo. Basi nilimpigia mke wake simu, nami nikasema, “Sikuweza kumpata mke wangu; ameenda dukani.” Ndipo nikasema, “Mwambie amwambie Ndugu Tony Stromei,” ambaye alikuwa ndiye rais wa tawi, “nisipokuwepo hapo Jumapili, amweke mhubiri mwingine tayari, kwa sababu huenda nisiweze kuondoka hapa kabisa. Nipo pamoja na wanaume hawa.”

¹²⁵ Ndipo kukatokea nini? Ninii... Usiku huo hakukuwa na theluji. Asubuhi iliyofuata, mawingu yalitanda sana na yenye hasira. Nikasema, “Sasa, ndugu, nimechunga ng’ombe hapa ndani, kwa miaka, na kuongoza. Tone dogo la kwanza la mvua, rudini kwenye kambi haraka mwezavyo, maana katika dakika kumi na tano nimeona wakati usingeweza kuona mkono wako mbele yako, kwa siku mbili ama tatu, kwa wakati mmoja, dhoruba inayopinda.” Hiyo ni futi elfu tisa pale pale. Tena nikasema, “Nyinyi, nyinyi mtakuwa tu ndani ya dhoruba, na mtapotea, na mtakufa hapa milimani. Sasa tutatoka...” Nilimweka kila mtu, nami nikarudi juu ya kilele. Ndipo nikasema, “Sasa, nisiponinii... Msiningojee kuingia ndani. Harakisheni tu mara tu inapoaanza; chembe ndogo ya kwanza ya mvua, kimbieni upesi kwenda kwenye kambi, na kwa sababu hamtaweza kuipata njia ya kurudi.” Walisema wangefanya hivyo.

¹²⁶ Nilipanda juu. Mbwa mwitu wakipiga makelele kila mahali, nami nilijua hali ya anga ilikuwa inaenda kubadilika. Ndipo, mara moja, mlipuko mkubwa wa upepo ukaja, na mvua ya theluji ikaanza kunyesha. Ndipo nikasema, “Nadhani kila mtu anarudi.”

¹²⁷ Vema, nilisimama na kuangalia kote. Nikawaza, “Laiti ningaliweza kumpata huyo kulungu kabla sijarudi, kwa sababu theluji itamfunika, na hawatapatikana tena mpaka majira ya kuchipua.” Kwa hiyo nikawazia, “Nilimsaka sana huyo kulungu.” Naye alikuwa ndiye kulungu wa kwanza niliyewahi

kumwacha aende namna hiyo, tangu niwe na bunduki hii ndogo, niliyoua wanyama hamsini na tano kwayo. Ndipo nikawaza, “Vema, sasa, ni—ninachukia tu kumwona akitoweka namna hiyo.”

¹²⁸ Ndipo kitambo kidogo tu, matone makubwa mno ya theluji, yalionekana kama ratili ishirini na nne, yakianguka tu kila mahali, ndipo upepo ukaanza kuvuma, na ilikuwa vigumu kwangu kuona jinsi ya kutoka juu ya kilele hiki. Nami nilijua kukaa juu ya mgongo huu wa mlima. Na iwapo ningeshuka na kufikia ghuba ndogo, ningeteremka kwenye hiyo ghuba mpaka nifikie kidaraja cha mguu, ndipo ningepapasapapasa kutafuta njia yangu ya kwenda juu mpaka nifikie mahali hema lilipokuwa. Hiyo ndiyo njia tu ungaliweza kutoka. Basi kwa hiyo nikawazia, “Kama nikisogea kwa njia moja ama nyingine, kwisha, hutapatikana, kwa hiyo utafia pale pale ndani.”

¹²⁹ Kwa hiyo nikaanza kuteremka chini ya mlima, ndipo nikafika chini yapata, loo, nakisia, yadi mia tatu, au mia nne, kutoka nilipokuwa.

¹³⁰ Sasa, hii yasikika ya kushangaza. Bali ninayo Biblia imewekwa hapa mbele yangu, Baba wa Mbinguni akinishuhudia. Karibu nikiwa mbioni, kujaribu kuepuka, upepo ulikuwa ukivuma kwa nguvu sana pale juu, nami ningeweza kuona yapata futi ishirini mbele yangu, katika vichaka nilivyokuwa ndani yake, miti, nao upepo ukivuma na kupinda. Ndipo Sauti ikasema, “Simama! Rudi mahali ulipotoka.”

¹³¹ Vema, nikasimama. Nikawaza, “Labda hiyo ilikuwa tu ni sauti ya huo upepo. Sikuwa nikiwazia chochote namna hiyo.” Ndipo nikangojea kwa dakika moja.

¹³² Na mmoja wa hao wavulana alikuwa ameniandalia sandiwichi, nami nikaitoa, na ilikuwa ni sandiwichi kwelikweli; nami, kukinyesha huku ninatokwa jasho, lilikuwa tu ni bongwe kubwa la—la mkate likiwa na nyama ndani, mahali fulani. Vema, ki—kidogo nilikuwa na njaa, kwa hiyo nikala, kwa vyovyote vile. Nami nilikuwa nimesimama pale. Ndipo nikakizika kile kijipande kidogo cha karatasi; kwa hiyo, mnyama ataviona vitu hivyo, na, chochote kilicho ustaarabu, wanakimbia na kutoroka.

¹³³ Kwa hiyo nikasimama hapo kidogo, ndipo nikawazia, “Vema, nitaendelea tu.”

¹³⁴ Nikaanza kwenda. Ndipo dhahiri tu kama mnavyoisikia sauti yangu, Kitu fulani kikasema, “Geuka na urudi mahali ulipotoka.”

¹³⁵ “Huyo angeweza kuwa ni Mungu akiniambia niingie katika mtego huo wa mauti?” Nikasimama hapo kwa dakika moja, ndipo nikawaza, “Huyo ni yeye Yule alisema kuhusu wale kuchakulo.”

¹³⁶ Yule yule niliyewaambia kumhusu jana usiku, kuhusu mke wangu; sauti tu, sauti tu ya kibinadamu. Yule yule aliyeniambia, nilipokuwa mvulana mdogo, “usinywe pombe wala kuvuta sigara,” na mambo haya yatakayotukia katika siku za mwisho. Mungu, nami nikisimulia haya huku Biblia ikiwa juu ya moyo wangu, ingenifaidi nini kuwaambia jambo lisilo sahihi na kujua kwamba naipeleka nafsi yangu kuzimu? Mnaona? Ni kweli. Si la kawaida, bali ni kweli.

¹³⁷ “Vema,” nikawaza, “Ninajua vya kutosha kuitii Sauti hiyo. Ni kwa nini mimi. . . Yeye anayo sababu fulani kwangu kuenda huko juu. Labda ni wakati wangu kuondoka.”

¹³⁸ Kwa hiyo nikageuka, na kupenya kupitia nyikani mpaka nikafikia kule juu kwenye mgongo tena, juu kabisa, labda yadi mia tatu, mia nne juu, moja kwa moja juu ya mlima, namna hiyo tena. Na ilikuwa nzito sana huko juu wakati huo, nisingeweza kuona chochote; upepo, nayo miti ikiinama tu na kujipinda.

¹³⁹ Ndipo nikaichukua bunduki yangu, nilikuwa nimevaa shati jekundu na kofia nyekundu, nikaweka bunduki, nisije nikaifanya da—darubini kujaa moshi ndani yake, kwa sababu dubu na kadhalika hutembea nyakati kama hizo, na pia simba; na kama ningekumbana na mmoja, darubini ilijaa moshi. Ndipo nikaishikilia tu juu namna hii, si karibu nami, mahali ingejaa moshi, bali kuzuia ukungu usiingie ndani yake, na unyevu kutoka kwenye theluji. Ndipo nikaketi chini ya mti.

¹⁴⁰ Nilikuwa nimeketi pale. Nikawazia, “Vema, ni kwa nini Yeye angetaka nje hapa juu? Ni—ninashuku sana kama ninaweza kupata njia ya kushuka chini sasa, ninii. . . ikiendelea kuwa ya kutisha sana.” Niliweza kuona yapata futi kumi au kumi na tano, labda, na hata si umbali huo, wakati mwingine si zaidi ya futi tano, na inazidi kuwa kali wakati wote. Vema, ni—nikawaza, “Vema, Yeye alisema nirudi. Yote niyuayo kufanya ni kuketi hapa.” Na theluji wakati huo karibu inchi moja, ama inchi moja na nusu, labda inchi mbili, juu ya nchi. Ilikuwa imechukua dakika ishirini ama thelathini. Na—na ilikuwa inavuma kwa nguvu, ilikuwa inaipeperushia mbali, pia. Nami nikaketi tu hapo kwa muda mfupi.

¹⁴¹ Nikasikia Sauti. Akasema, “Mimi ndimi Mungu wa Mbinguni, aliyumba mbingu na nchi.”

¹⁴² Nikaivua kofia yangu upesi, kofia, halafu nikakaa tu kimya. Ndipo nikasikiza tena. Nikawaza, “Huo haukuwa upepo.” Loo, ulikuwa unavuma, ukipiga kelele.

¹⁴³ Ndipo nikaisikia tena. Kasema, “Mimi Ndiye Yule aliyetuliza upepo juu ya bahari kuu. Mimi Ndimi, Muumba. Niliwaumba kuchakulo mbele yako. Nilifanya mambo haya.”

Nikasema, “Naam, Bwana. Ninakuamini Wewe.”

144 Kasema, “Simama kwa miguu yako.” Nikasimama, kwa miguu yangu. Akasema, “Sasa nena na dhoruba. Itafanya kile utakayoambia ifanye.”

145 Sasa, hiyo ni kweli. Mimi, nitakapokutana nanyi kwenye Hukumu, itanibidi kujibu kwa haya yote. Niliwazia Yeye. . .

146 Nikasema, “Dhoruba, nenda mahali pako, koma. Na, jua, wewe angaza kikawaida kwa siku nne.”

147 Na punde tu niliposema hivyo, mvua ya theluji na mawe, ambayo ilikuwa nusura iniangushe kwa upepo, ilikoma mara moja. Ndipo kwa dakika moja ama mbili, jua lilikuwa linaangaza moja kwa moja, juu yangu. Ndipo nikaangalia chini kupitia milimani, nikaona u—upepo wa mashariki ukija. Upepo ulikuwa unakuja kutoka magharibi. Upepo wa mashariki ukaja, na ulikuwa unakuja upande huu, na ningeweza kuona mawingu kiajabu tu. . . Mahali yalipoenda, sijui.

148 Nami nikasimama pale kwa dakika chache, machozi yakitiririka kupitia ndevu zangu, nazo zikiwa na mvi. Nikawaza, “Mungu, kwa njia gani, sijui la kufanya.”

149 Nikawaza, “Vema, nilikuwa. . . Nadhani ndugu hao wote wamerudi kwenye hema. Nalo jua likiangaza kila mahali.”

150 Nikaanza kuteremka chini mlimani. Na theluji yote ikikauka, kwa hilo jua kali; mvuke ukitoka kwenye shati langu. Tofauti, ya dakika moja tu, ama mbili. Nikaanza kutembea kushuka chini ya mlima. Ndipo nilipofanya hivyo, nikasema. . .

Nilisikia Sauti ikisema, “Kwa nini usitembee pamoja na Mimi?”

151 Nikasema, “Bwana, majaliwa makuu kuliko yote niliyowahi kupata!” Nikageuka na kuanza kurudi chini kupitia njia kubwa za kulungu, chini kupitia msitu huo ambao haujaguswa bado.

152 Ndipo nikawaza, “Vema, nitaendelea kwenda huko chini mpaka mahali ambapo mimi humpigia saluti Meda, mke wangu.” Nami nilikuwa ninaenda pale kama, yapata nusu saa, robo tatu, baadaye. Theluji ilikuwa imekauka yote na kutoweka.

153 Basi nikaanza kuwazia, “Sijui ni kwa nini mke wangu hajawahi kuniambia chochote kuhusu kwenda.” Nikasema, “Ninakumbuka nilipompeleka huko juu kwa mara ya kwanza na kumnyanyua kuruka hayo magogo, tulipokuwa tumeoana.” Nikasema, “Sasa ana mvi.”

154 Nikamaka, “Uhm!” Ndevu zenye mvi usoni mwangu, nyeusi na zenye mvi zikichangamana pamoja. Nikawaza, “Bill, huna muda mwingi zaidi. Unazeeka.”

155 Kisha nikaanza kusonga. Ndipo nikaangalia juu, ilionekana kana kwamba ningeweza kumwona amesimama mbele yangu pale, huku ameinua mikono yake, angali na kichwa cheusi.

156 Nikainamisha kichwa changu chini. Nilikuwa nikipanda kwenda juu mahali padogo ambapo baadhi ya miti mitetemo, na kuna njia ndogo iliypinda kwenye ninii... Niliinamisha tu kichwa changu kuegemea tawi, namna hii. Nami nilikuwa nimesimama pale, nikilia, na ningeweza kusikia kitu fulani kikienda, "Pat, pat, pat." Ndipo nikaangalia chini; yalikuwa ni maji yakitoka machoni mwangu, kupitia ndevu zangu, yakianguka kwenye majani makavu; ambapo, yapata dakika thelathini zilizopita, kulikuwa na inchi moja ya theluji, huku kukivuma dhoruba kali.

157 Niliposhuka chini kutoka mlimani, siku nne baadaye; hamna hata wingu moja angani, kwa siku nne baadaye. Nikaingia, na kumwambia mtu wa kituo cha petroli, "Je!... kumekuwa kukavu kabisa?"

158 "Naam." Kasema, "Unajua, kitu cha ajabu sana, tulibashiriwa dhoruba hivi majuzi, na, unajua, ilikoma ghafla."

159 Halafu basi nikaja kufikia mpaka wa New Mexico, nikirudi Arizona. Ndipo nikamwambia Billy, mwanangu, nikasema, "Hebu tuingie hapa ndani na tuone tu kama ilikuwa huku chini."

160 Nikasimama hapo ndani. Ilikuwa ni Jumapili asubuhi. Nikanunua ninii... Nikanunua petroli. Naye mtu huyo akasema, "Vema, mmekuwa mkiwinda?"

Nikasema, "Naam, bwana."

"Bahati yoyote?"

161 Nikasema, "Naam, bwana, tulikuwa na wakati mzuri." Nikasema, "Kunaonekana kukavu sana."

162 Naye akasema, "Naam, kumekuwa kukavu sana kote hapa." Akasema, "Tuliahidiwa theluji kubwa hivi majuzi." Tena kasema, "Unajua, dhoruba hiyo kweli ilianza, na kwa njia moja ama nyingine ikatoweka." Loo, jamani! Loo, jamani!

163 Nilikuwa nimesimama kuegemea kando ya mti huu. (Katika kufunga.) Nikiwa nimesimama kando ya mti huu, nayo machozi yakidondoka kutoka machoni mwangu. Nikawaza, "Mungu!"

164 Wazia tu, Mungu yeye yule aliyesema, "Amani, tulia," kwa mawimbi, na dhoruba zikamtii, Yeye angali ni Yesu yeye yule yupo papa hapa mwituni pamoja nasi. Yeye angali ni Neno. Neno, maumbile yote hayana budi kulitii Neno Lake, kwa kuwa Yeye ndiye Muumba wa maumbile.

Nikasimama pale, nayo machozi yakidondoka kutoka mashavuni mwangu.

165 Na kwa yapata miaka mitano sasa, sijakuwa katika huduma za nje, nikienda tu kwenye makanisa na chochote nilichoweza. Nyote mnajua hilo. Na moyo wangu umekuwa na mzigo. Ningeenda hapa nje, kuja Arizona. Naye angeniambia mambo ya kufanya, ningeenda na kuyafanya, lakini inaonekana

kama uamsho umeisha. Nami nisingeweza . . . sijui kilichokuwa kikiendelea. Moyoni mwangu, ningetubu. Ningesema, “Bwana, kama nimefanya chochote, niambie; nitasahihisha.” Nikiwa na mzigo wakati wote, hisi ya kutisha kabisa, na nisingeweza kuwa na ushindi niliotaka.

¹⁶⁶ Mambo mengi makuu Yeye alikuwa amefanya na kuonyesha, ambayo nyinyi nyote ni mashahidi, nikija hapa na kuwaambieni kuyahusu, kuona magazeti yakiyaandika, na majarida, na kadhalika, kuhusu mambo makuu ya kimbinguni ambayo yameonekana na kufanywa.

¹⁶⁷ Lakini moyo wangu ulikuwa ungali mzito. Nami nilikuwa nimeegemea kwenye kichaka, namna hii tu. Ndipo nikawaza, “Mungu mkuu wa Mbinguni. Jua hilo lenye joto likiniangazia, hapana wingu mahali popote, na dakika chache zilizopita Wewe ulininii—Wewe ulilikanusha tu neno la mwanadamu. Maumbile yalifanya hivyo. Ingewezaje kufanywa, Bwana? Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ilikuwa ni Neno Lake ambalo Wewe ulinifanya tu kulinena.” Nikawaza, “Baba, jinsi nilivyo na shukrani!”

¹⁶⁸ Nikasikia kitu kikienda . . . [Ndugu Branham anagonga mara mbili kwenye mimbara—Mh.] Ndipo nikaangalia; wakisimama moja kwa moja mbele yangu walikuwa kulungu wawili, watatu, nao walikuwa wakiniangalia. Sasa, kulungu hao walikuwa wametupiwa risasi, sana, katika juma lililopita, na kulikuwa na wawindaji humo ndani. Nami hapa nilivaa nyekundu; mtu yeyote anajua [Ndugu Branham anadata kidole chake] kwamba wameenda upesi hivyo. Bali walikuwa wakiniangalia.

¹⁶⁹ Tena, kwa kulungu wa kuliwa, hakungeweza kuwa na yeyote bora. Alikuwa ni kulungu jike mkubwa, watoto wawili wa kulungu waliokomaa. Ndipo nikawaza, “Hiyo ni sawa tu! Tunahitaji kulungu watatu.”

¹⁷⁰ Kitu fulani kikasema, “Unajua, Bwana amewaweka mikononi mwako.”

¹⁷¹ Lakini nilipokuwa na Wafanyabiashara wa Full Gospel, Ndugu Clayton, yapata mwaka mmoja hapo kabla, alienda pamoja nasi wakati nilipomshika yule samaki mkubwa wa kumbukumbu. Mwaka huo, kwa ajili ya watu, niliwaua kulungu kumi na tisa wa kaskazini. Nami . . . ninii . . .

¹⁷² Wakati mwingine, wafanyabiashara . . . Samahani hili, ndugu zangu. Baadhi yao ni madaktari, na, mwajua, hawawezi kutembea; na wanene, mwajua, na wengi wameketi kwenye dawati. Wanasema, “Billy, niletee mmoja wa miaka miwili. Niletee ng’ombe wa bluu. Ninataka dume la paa. Niletee cha—chano kizima.” Vema, nilikuwa tu na yubile kule nje, nikipiga risasi, kuwaua kulungu na kadhalika.

¹⁷³ Lakini Bwana aliniambia nisifanye hivyo. Nami nilimwahidi, katika ile dhoruba kali kule Colorado, si . . . miaka

kabla ya hapo. Nikasema, “Bwana, nitawaongoza watu kwenye wanyama, bali si kuwaulia watu wanyama tena.” La. Isipokuwa iwe ni dharura na inatubidi kumpata.

¹⁷⁴ Na kama mnakumbuka, enyi wavulana, usiku kabla hatujaondoka. Maskini ndugu pale chini, ambaye hakuwa amepata kulungu. Jina lake ni nani? Palmer, akaja, na kuweka zaka ya dola kumi mkononi mwangu. Akasema, “Ndugu Branham, hizi ni zaka zangu, ziweke kanisani.” Akasema, “Hivi utaniletea kulungu?” Loo!

Ni—nikasema, “Vema, mimi, Ndugu Palmer, ni—ni—nitafanya niwezayo.”

¹⁷⁵ Halafu basi huko juu, Ndugu Evans alihitaji kulungu, na papo hapo mbele yangu walisimama wale kulungu watatu; nilikuwa na hii bunduki yangu begani mwangu. Nikavuta tu bega langu namna hiyo. Nikawaza, “Hawawezi kutoroka kutoka kwangu. Wapo papa hapa.” Nilikuwa mwepezi sana na bunduki. “Ninaweza kuwaua wote watatu kabla hawajageuka.” Mnaona? Nami nilikuwa na bunduki. Nikawaza, “Hao hapo, sawa.” Nikaivuta tu bunduki upesi. . .

¹⁷⁶ Kisha ikawa kwamba niliwazia kuhusu ahadi hiyo. Nikasema, “Siwezi kufanya hivyo. Siwezi kufanya hivyo.” Nikasema, “Ninakumbuka wakati mmoja ambapo mtu alimwambia mwenzake, ‘Mungu amemtia Yoabu mikononi mwako, ama Sauli,’ Yoabu alimwambia Daudi. Daudi akasema, ‘Mungu aniepushe nisimguse mtiwa mafuta Wake.’ Hiyo ilikuwa ahadi yangu, kwamba nisingefanya hivyo.”

¹⁷⁷ Nikawaza, “Wako moja kwa moja juu ya kilima hiki. Ninaweza kuwabingirisha moja kwa moja huko chini; tuweze kuwachukua kwa urahisi. Kulungu watatu wa kupendeza wamesimama pale!”

Nikasema, “La, siwezi kufanya hivyo.”

¹⁷⁸ Na hapa hawa wakija juu namna hiyo, watoto wa kulungu, wawili wakubwa, wa kiume na wa kike, na mama kulungu. Nao wakaja, wakitembea, wakiangalia huku na huku, jamaa wakubwa wanono.

¹⁷⁹ Ndipo nikasimama pale kidogo. Nami nikawaza, “Hiyo si kawaida, kwa kulungu, nami nimevalia kitu chekundu namna hiyo.” Nikawaza, “Nitawatisha.”

¹⁸⁰ Nikasema, “Mko mikononi mwangu! Msingeweza kutoroka hata mfanye nini, bali sitawadhuru. Endeeleni!” Walitazamana tu, na wakaendelea kuja. Na wakafika karibu sana nami, wakinitazama.

¹⁸¹ Vema, nikaiweka bunduki chini. Nikasema, “Mama, wachukue watoto wako na uendeleo huko mwituni. Nipo hapa ninaburudika katika Uwepo wa Mungu. Niliahidi kwamba nisingeua wanyama kwa ajili ya wengine.” Nikasema,

“Sasa wewe wachukue watoto wako ukaende mwituni. Mimi ninapenda huo mwitu, pia. Nenda huko nje!”

¹⁸² Akaniangalia. Na wote wawili wakaangalia kote, wote watatu. Ndipo wakageuka na kuondoka, kisha wakarudi tena.

¹⁸³ Ndipo nikasema, “Sitawadhuru.” Nikasema, “Nendeni mkaingie mwituni. Mko mikononi mwangu. Msingeweza kuponyoka. Bali,” nikasema, “Nimekuwa mikononi mwa Mungu, na hata hivyo nisingeweza kuponyoka, pia. Aliniachilia. Nilimtolea ahadi. Ninawaachilia. Nendeni, mwe na wakati mzuri, mfurahie misitu hii. Ninaipenda. Nyinyi endeleeni!”

¹⁸⁴ Wakasimama hapo kwa kitambo kidogo, kisha wakaja karibu kabisa, hata wangekula kutoka kwa mikono yangu; wakageuka na kuniangalia wote, namna hiyo, kisha wakaondoka. Wakasimama na kuangalia nyuma tena, wakaenda moja kwa moja kuingia mwituni. Nami nilikuwa nimesimama pale. Nikawaza, “Hilo si kawaida, kwa kulungu. Sijui kama ni kwa sababu Bwana Yesu yupo hapa, Uwepo Wake?”

¹⁸⁵ Na papo hapo Sauti ikanena nami, kasema, “Ulikumbuka ahadi yako, sivyo?” Nilijua ilikuwa ni Yeye.

Nikasema, “Naam, Bwana.”

¹⁸⁶ Akasema, “Ndivyo Nami nakumbuka Yangu. Sitakuacha kamwe. Sitakupungukia.”

¹⁸⁷ Mzigo huo ukainuliwa. Enyi marafiki Wakristo, haujarudi tangu wakati huo. Hiyo ilikuwa ni Oktoba iliyopita. Nimekuwa ni mtu tofauti.

¹⁸⁸ Timiza ahadi yako kwa Mungu. Lolote unalomwambia Mungu, liamini. Jitenge na chochote kinyume na Neno Lake. Mungu atasikia na kujibu maombi.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

¹⁸⁹ Je! uko tayari kujitenga mwenyewe, usiku wa leo, kutokana na kutokuamini kote, kusikia Neno la Bwana? Kama utafanya hivyo, na kuamini kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Mambo haya aliyohidi kufanya, tunamwona akiyafanya. Je! mtainua mikono yenu na kusema, “Mungu, ninakutolea Wewe ahadi usiku wa leo. Ninaamini kila kitu ambacho Wewe uliahidi. Ninaamini kila Neno; hata sitatilia shaka tena?”

¹⁹⁰ Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unajua hadithi hii kuwa ni kweli. Hiyo ilikuwa ni mara ya nne. Na halafu mara ya tano, ilikuwa kwa mke wangu wa thamani, wakati Wewe... Juma lililopita, wakati yule daktari akiandika ile taarifa, kile kivimbe kikubwa kilitoweka kabla ya mkono wake kumgusa; sawa tu na ilivyo sema.

¹⁹¹ Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utawasaidia watu hawa. Ninatambua kwamba ninazeeka. Ninajua kwamba lazima niondoke karibuni. Nami ninaomba, Bwana, kwamba, nijalie

niwe mnyofu na mwaminifu kwa ndugu zangu, nijalie niwe mnyofu na mwaminifu kwa watu Wako. Ikiwa siwezi kuwa mwaminifu kwao, basi sidhani ninaweza kuwa mwaminifu Kwako, Bwana, maana ninataka kutoa ushuhuda Wako. Pia ninaomba ya kwamba Wewe utajalia Neno liishi sana ndani yetu, usiku wa leo, hata utatujalia sote imani. Na kwa karama hii ndogo ambayo...

¹⁹² Watu hufikiria wakati mwingine kwamba karama ni kitu ambacho unaweka mikononi mwako, na kuondoka na kwenda huko nje na kukata ukipenya. Karama si hicho, Baba. Jalia waelewe kwamba karama ni kujiondoa mwenyewe njiani, kusudi Roho Mtakatifu aweze kufanya kile Yeye atakacho kufanya.

¹⁹³ Bwana, jalia tujiondoe njiani sasa, na hebu Roho Mtakatifu mkuu aje na kufanya kazi kupitia sisi. Pia jalia tuone, usiku wa leo, ahadi za Yesu Kristo, kwamba... Yule niliyemrejea hasa usiku wa leo, Bwana, kwamba, Yule ambapo Mungu alishuka mbele ya Ibrahimu, akadhihirishwa katika mwili, na kutambua siri ya moyo, Huyu alikuwa ni Mungu. Ndipo wakati Yeye alipofanyika mwili akakaa katikati yetu, Yeye alitambua siri ya moyoni. Nayo Biblia inasema kwamba, "Neno la Mungu huyatambua mawazo yaliyoko moyoni." Hivyo ndivyo wanafunzi walivyojua kwamba Yeye alikuwa ni Mungu.

¹⁹⁴ Sasa, Baba, hivi Wewe utakuja usiku wa leo na kuruhusu maskini maskini zetu duni ziwekwe wakfu Kwako, kwamba Wewe utatufanya tuamini, kwamba ni Roho Wako aweze kujitambulisha miongoni mwetu usiku wa leo, kwamba Wewe ungali ni Neno. Ndipo tutajitenganisha wenyewe kutoka kwa kutokuamini kote na kukufuata Wewe. Katika Jina la Yesu, naomba Wewe utunenee. Amina.

[Mtu fulani anatoa himizo—Mh.]

¹⁹⁵ Mungu mkuu wa Mbinguni, turehemu. Tusaidie, Ee Bwana, kuzitii Amri Zako. Na ututumie kwa heshima Yako. Nasi tunakushukuru kwa maneno haya yanayotia moyo. Sasa jalia Roho Mtakatifu atembee kupitia sisi na kuthibitisha maneno haya. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹⁹⁶ Iweni na imani katika Mungu. Msitie shaka. Iweni na moyo wa ushujaa. Wakati wa Kuja Kwake unakaribia.

¹⁹⁷ Sasa, usiku wa leo, tuna makundi ya kadi za maombi. Ni wangapi humu ndani walio na kadi za maombi, inueni mikono yenu. Ingekuwa vigumu kwangu kupitia kundi hilo pamoja na utambuzi, kama Bwana atatupa huo. Lakini hebu nichukue tu muda mfupi na niseme hili, ni wangapi humu ndani ambao hawana kadi za maombi, na unaomba ya kwamba Mungu atakuponya? Sasa hebu Bwana Mungu na asaidie kila mmoja wenu.

¹⁹⁸ Mimi ni ndugu yenu. Yesu ni Mwokozi wenu. Mungu ni Baba yetu. Sisi ni watu. Sisi si wa ulimwengu huu, wakati tunapozaliwa na Mungu, sisi ni wa Juu. Sasa, kabla hatujawa na mstari wa maombi, kuwaomba wagonjwa. . . Na yupo mtu hapa jukwaani, usiku wa leo, ambaye huwaomba wagonjwa, pia, na wahudumu huko nje wanaowaomba wagonjwa. Sitaki kuacha dhana kwamba mimi ndiye pekee ninayewaomba wagonjwa. Mnaona? Mungu haninii. . . Si lazima anitumie. Yeye angeweza—Yeye angeweza tu kukutumia wewe au yeyote yule. Jambo ni, kuamini yale Yeye aliyosema kuwa ni Kweli.

¹⁹⁹ Bali sasa, kama nilivyosema katika thibitisho la yale yaliyosemwa, hebu tuinamishe tu vichwa vyetu kwa muda mfupi tu. Ninyi mnaoomba, nanyi ni wagonjwa wala hamna kadi za maombi, nyinyi ombeni na kusema jambo kama hili: “Bwana Yesu, ninajua Biblia inasema kwamba maombi ya imani yatamwoko mgonjwa; Mungu atamwinua. Na pia imesema kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

²⁰⁰ Kama Yeye ni yule yule, vema, basi itambidi kutenda vile vile, afanye lile lile. Na basi tena, Biblia ilisema kwamba Ne—Neno la Mungu lilikuwa kali kuliko upanga ukatao kuwili, na lilitambua mawazo yaliyokuwa moyoni. Tunajua kwamba wakati Neno lilipofanyika mwili, katika Utu wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, hilo hasa ndilo Mungu alilotenda kupitia Mwanawe. Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 14, “Kazi nizifanyazo nyinyi nanyi mtazifanya, hata kubwa zaidi na nyingi, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu.”

²⁰¹ Na sasa Biblia inasema, pia, katika Kitabu cha Waebrania, kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu sasa. Je! sisi sote tunaamini hilo? Hakika. “Yeye ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Sasa, “Yeye ndiye.” Si mimi ndiye; Yeye ndiye. Hakuna mtu ambaye ndiye. “Yeye sasa ndiye Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.”

²⁰² Sasa, kama unajisikia na uko tayari kujitokeza na ukajiweka tu huru, na kutokuamini kwako kwote, na kusema, “Hebu nikuguse Wewe, Kuhani Mkuu mashuhuri!” Sasa, ikiwa Yeye ni Kuhani Mkuu, na ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye atatenda kama alivyotenda wakati ule, kwa sababu ni Yeye yule.

²⁰³ Mwanamke alingusa wakati mmoja wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, kwa njia ya kuonekana, kwa mkono wake. Yeye aliuhisi mguso huo, akageuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa?” Na wote wakakana. Bali Yeye alitambua mawazo, ndipo Yeye akampata mwanamke huyo, akamwambia kilichokuwa shida yake, na imani yake ilikuwa imemponya.

²⁰⁴ Sasa, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Labda mwanamke huyo hakuwa na kadi ya maombi, bali alikuwa na imani. Na hiyo tu ndiyo inayohitajika. Kuwa na imani. Mguse Tabibu mkuu. Na kwa karama ya Kiungu, iwapo tu ninaweza

kujiondoa mwenyewe njiani, nimwache Roho Mtakatifu kusema yale Yeye anayotaka kufanya, na kufanya yale anayotaka kufanya. Na hiyo ni karama, si tu cha kuwazia. Kama ni cha kuwazia, hakitafanya kazi. Kama ni halisi, hufanya kazi. Hilo ndilo Yesu alisema, “Si Mimi nifanyaye kazi, ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu.” Kwa hiyo, isingeweza kuwa ni mimi. Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu; mimi ni mwenye dhambi, aliyeokolewa kwa neema Yake.

²⁰⁵ Amini tu. Usisukume. Amini tu, na kusema, “Bwana Yesu, nijalie niguse vazi Lako.” Omba tu rahisi. Endelea tu kuomba. Kila mtu kaa mahali ulipo, omba tu na uamini.

²⁰⁶ Amini tu, wala usiwe na haraka. Usijaribu kusukuma. Amini tu. Sasa je! mnaamini, kila mmoja? Je! mwaweza kuamini? Sahauni tu yote yaliyopita. Wazia kwamba Yesu aliahidi hili. Ninajua si kawaida, bali Yesu aliliahidi.

²⁰⁷ Sasa, mkipenda, iweni na kicho kwa muda mfupi tu, ndipo tutaanzisha mstari wa maombi. Sisemi kwamba atafanya hili. Huenda akafanya. Kwa neema ya Mungu, ni—nimewekwa huru kutokana, nafikiri, kutokana na mawazo yangu mwenyewe. Naomba Yeye. . .

²⁰⁸ Sasa wewe, kama unajisikia kuinua kichwa chako na uangalie tu upande huu, na uwe katika maombi. Kama vile Petro na Yohana walivyosema, “Niangalieni mimi,” sio, “tuangalieni sisi,” hasa, hawakumaanisha. . . Kuzingatia tu yale waliyokuwa wanasema.

²⁰⁹ Sasa nyinyi ni wasikilizaji. Karibu hakuna mtu hapa nimjuaye, kando na—na hawa wavulana wa Martin wanaoketi hapa. Na ninafikiri huyu ni Ndugu Daulton anayeketi hapa chini, sina hakika, huku umevaa miwani yako yenye rangi. Nitajaribu kuwapita hapo, watu nisiowajua.

²¹⁰ Vema, sasa naomba Yesu Kristo aje pamoja na nguvu Zake, ili mweze kuona ya kwamba ahadi ya siku hii, Maandiko yaliyotabiriwa ya siku hii, hata kulingana na Malaki 4, hayana budi kutimizwa. Kitu fulani hakina budi kufanya hivyo. Mungu ameahidi hivyo.

²¹¹ Yupo mama aliyeketi moja kwa moja hapa nje. Yuko njiani mwake kuelekea hospitalini kesho. Amekuwa kwenye ajali, ajali ya motokaa. Ameumia, ana matatizo ya ndani, mkono ulioumia. Huna ninii. . . Je! una kadi ya maombi, mama? Huna. Je! mimi ni mgeni kabisa kwako? Sikujui. Hatufahamiani. [Dada huyo anasema, “La, bwana. Nimekusikia ukihubiri.”—Mh.] Mama? [“Nimekusikia ukihubiri.”] Umenisikia tu nikihubiri, bali unajua sijui chochote kukuhusu wewe. Je! mambo hayo ni kweli? Kama ni hivyo, inua mkono wako. Mungu akubariki. Vema, bwana. Kuwa na imani, haitakubidi kwenda. Shida yako imekwisha.

Mama huyo aligusa nini?

212 Yupo mwanamume aliyeketi moja kwa moja nyuma yake. Hamwezi kuiona hiyo Nuru? Angalieni hiyo Nuru ya rangi ya kaharabu ikisonga. Ni mwanamume aliyeketi moja kwa moja nyuma ya huyo mama. Anaomba kwa ajili ya jambo fulani; ni ndugu aliye hospitalini. Je! unaamini kwamba Mungu atamponya ndugu yako, amrejeshee akili yake timamu na kila kitu, kumfanya sawa? Je! unaamini hilo? Mimi ni mgeni kwako. Hiyo ni kweli? Hiyo ndiyo ha- . . . Amini! Vema, unaweza kuwa na . . .

Huyo aligusa nini?

213 Huyu hapa mama, moja kwa moja nyuma ya hiyo, aliyeketi hapa nyuma. Yeye ni . . . Mnaona hiyo Nuru, mnaweza kuona Hiyo? Angalieni *hapa*. Angalieni, kila mtu aangalie, ona papa *hapa*, namna ya Duara inayoonekana ya kaharabu. Moja kwa moja chini Yake yupo mama. Yeye yupo hapa, anaomba kwa ajili ya mtu fulani. Ni watoto wawili, mjukuu, kitukuu. Mama huyo hatoki hapa. Anatoka California, na amekuja hapa akitaka maombi.

214 Pia, kuna mtu pamoja naye. Ni dada yake. Yeye huketi moja kwa moja hapa nyuma, amevaa hilo gauni jekundu. Ana kifafa. Hiyo ni kweli. Anatoka California, nawe ulimleta pamoja naye. Jina lako ni Mary. Unaamini kwa moyo wako wote. Je! mambo hayo ni kweli? Punga mkono wako kama ni kweli. Je! unaamini kwa moyo wako wote? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Basi unaweza kupata ulichoomba. Sasa, yeyote anayetaka kuwauliza watu hao kama niliwajua. . . Je! una kadi ya maombi, mama? Huna? Huihitaji.

215 Hapa, hapa yupo mtu aliyeketi moja kwa moja hapa nyuma, akiniangalia, kwenye mwisho wa safu. Ana shida na magoti yake. Kama angeamini kwamba Mungu atayaponya hayo magoti, anaweza kupata kile anachoombea. Je! unaamini? Vema, shida yako ya magoti imeisha, bwana. Je! una kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi? Huihitaji.

Sasa, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele!”

216 Mama aliyeketi hapa, ana tatizo la kike. Je! unaamini? Naam, mama huyo. . . Loo, jamani, atalikosa. Mwenye koti jekundu. Jina lake ni Bi Daily. Amini kwa moyo wako wote. Bwana Yesu Kristo anakuponya, Bi Daily.

217 Uliza kama ninamjua mama huyo. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Baba wa Mbinguni anajua hilo.

Unasema, “Kwa nini ulimwita, jina lake?”

218 Vema, Yesu alisema, “Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona.” Je! hiyo ni kweli? Sasa, huyo si ni Yeye, yule yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! mnaamini hilo kuwa ni kweli? Sasa, Yesu alisema nini? Hili litatendeka.

219 Pia, kumbukeni, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho iliyotolewa kwa Kanisa teule, Ibrahimu na kundi lake, kabla mwana aliyeahidiwa kutokea. Je! hiyo ni kweli? Mungu alikuwa amempa Ibrahimu ishara kote safarini, na vivyo hivyo amelipa Kanisa. Lakini wakati Malaika wa Bwana aliposhuka na kufanya hilo, Yeye aliwaangamiza Wamataifa wasioamini; ndipo mwana mtarajiwa, aliyekuwa amengojewa, akatokea, Isaka.

220 Huduma hii itamalizika hivi karibuni, ndipo Mwana anayetazamiwa atajitokeza, Mwenyewe. Kanisa limekuja kupitia kuhesabiwa haki, kupitia Walutheri; utakaso, kupitia wa Wesley; kuingia kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, kupitia Wapentekoste; na sasa linamalizia kwenye huduma ya Jiwe la kichwa, likifaninisha kila mara moja kwa moja hadi lile Kamilifu; kivuli kilichokuwa mfano kikifanyika kitu halisi, ndipo Yesu atakapokuja kulichukua Kanisa Lake, siku moja, hao wanaoamini.

221 Jitenge mwenyewe na kutokuamini, na uamini, usiku wa leo. Je! mtafanya hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

222 Hebu wale walio na kadi za maombi sasa, kuanzia... Naamini niliombea mpaka ishirini na tano, jana usiku. Je! hiyo ni kweli? Nafikiri hiyo ndiyo iliyoandikwa, namba moja, ishirini na tano. Sasa ishirini na sita, ishirini na saba, ishirini na nane, thelathini, pageni mstari *hapa*. Mkiwa na kadi za maombi namba moja, pageni mstari upande huu *hapa*. Mtafanya hivyo sasa?

223 Sasa, tuna mstari wa utambuzi bila kadi za maombi. Ili watu waseme nilikuwa nikisoma yaliyokuwa kwenye kadi zao za maombi, kulikuwa na... Watu hao hawakuwa na kadi za maombi. Ni watu tu walioketi hapo, na sasa inaendelea. Ni wangapi wamewahi kuona hiyo ikiendelea kwa nusu saa kwa wakati mmoja, au zaidi, namna hiyo, mnaona, na mambo yanatendeka. Lakini, mnaona, inatubidi kushikilia nguvu kidogo. Nina mikutano arobaini na kitu mbele yangu, kote kufikia huko Kusini.

224 Na sasa songeeni *hapa*, *enyi* mlio na kadi zenu za maombi, songeeni upande huu. Wote wenye kadi za maombi A, njoni upande *huu* *hapa*, kadi za maombi A.

225 Sasa, sisi tuliobaki, hebu tumwimbie Mungu, *Amini* Tu. Je! mtafanya hivyo? Sisi sote pamoja.

Amini... (Hayo tu. Amini tu kitu gani? Amini
Neno Lake)... amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu;
Amini tu...

Bwana... Bwana...

226 [Ndugu Branham anasema yafuatayo kwa mtu fulani aliye kwenye jukwaa—Mh.]: Labda kama ningekuwa moja kwa moja

hapo chini, labda ingekuwa bora? Je! tunaweza kwenda huko chini, tuwaombee wagonjwa? Kwenda *hapa* chini, kuwaombea wagonjwa? Inaonekana kama tunaweza.

227 Ni wangapi wanatamani watu hawa waweze kuponywa? Sasa, mnaona, uponyaji ni wa Mungu. Je! hiyo ni kweli? Sasa, kama Yesu angalisimama hapa usiku wa leo, akiwa amevaa suti hii aliyonipa, na alikuwa amevaa suti hii, Mwenyewe, ninii . . .

Kama ungesema, “Bwana, naomba Wewe uniponye.”

228 Yeye angesema, “Tayari nimekuponya.” “Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Je! hiyo ni kweli? Mnaona, Yeye amefanya hivyo tayari; ni katika wakati uliopita.

229 Unasema, “Bwana, niokoe.” Amefanya hivyo tayari. Haijalishi unalia kiasi gani, au kuomba, na kupigapiga kwenye dawati, haitakuokoa mpaka uamini na kukubali yale aliyokufanyia. Je! hiyo ni kweli?

230 Ni kitu hicho hicho. Mimi siwaponyi watu. Siwezi kuwaponya watu. Lakini Yeye angefanya nini, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Angefanya tu kile alichofanya sasa, kwa kuwa hicho ndicho Yeye aliahidi kwa ajili ya siku hii. Ni wangapi wanajua kuwa hicho ndicho Yeye alichohidi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye ameahidi. Naam, bwana. Aliahidi hicho, katika Maandiko yote. Nyinyi nyote chukueni kanda, *Nyakati Saba Za Kanisa*, na kadhalika, mwone mambo hayo yakithibitishwa kwa Maandiko, kwamba ni kweli.

231 Sasa, kwenu ninyi mnaosimama kwenye mstari huu wa maombi, kushuka kwenye mstari huo wa utambuzi. Yesu aliona ono moja, Naye akasema, “Naona kwamba nguvu zimenitoka.” Huo ni uweza. Hiyo ni kweli? Maono, uko katika ulimwengu mwingine. Sasa, Yeye yupo hapa. Huyu ni Yeye mliyemgusa. Mnaona? Sasa, inatambulisha tu kwamba Yeye yupo hapa pamoja nasi.

232 Sasa ni wangapi watakaoamini, kama tutatembea tu kupitia mstari huu, na kuniacha niombe na kuwawekea mikono, kisha urudi kwenye kiti chako? Je! mnaamini kwamba nikiwaombea hapa, na halafu niwawekee mikono, kila mmoja wenu atapona?

233 Je! mnaamini huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu hapa? Angeweza tu kuendelea kufanya hivyo. Kama mnataka kuachana na huo mstari, na kuendelea tu kwa mengine zaidi, mbona, tutafanya hivyo. Mnaona, hiyo ndiyo sababu, Roho Mtakatifu yupo hapa. Mnaona? Si ninii . . . Inategemea tu fi—fikira zako, kama ingekufanya uamini zaidi.

234 Lakini watu wengi wamefundishwa, “Wawekee mikono.” Biblia ilisema, “Yeye alilituma Neno Lake na kuwaponya.” Vema, hilo ndilo alilofanya sasa hivi, amelithibitisha Neno

Lake, akalituma kwako, akalithibitisha, na Hilo likawaponya. Mmataifa alisema...

Myahudi alisema, "Njoo, ukaweke mikono juu ya binti yangu, ataishi."

²³⁵ Mrumi alisema, "Sistahili Wewe kuja chini ya paa langu. Sema tu Neno!" A-ha. Hilo ndilo ninalojaribu kuwafanya kuamini, mnaona.

²³⁶ Bali kama unataka kuombewa, na kuwekewa mikono, sasa ninataka kila mmoja wenu kujiunga nami katika maombi tunapowaombea watu.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

²³⁷ Bwana Yesu, ninawaombea watu sasa. Wanajua kwamba Wewe unasimama hapa. Wanajua kwamba Wewe uko miongoni mwa watu. Basi watu hawa wanapopitia kwenye jukwaa hili usiku wa leo, jalia wasije, kuja tu karibu nami, mtumishi Wako, ama watumishi hawa wengine Wako wanaoketi hapa. Jalia watambue ya kwamba wanakuja kwenye hekalu la Mungu aliye hai, wanakuja chini ya ahadi ambayo Mungu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao watakaoamini. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Yeye aliahidi hilo. Aliahidi kwamba mtu yeyote ambaye angeamini angeokolewa, na kila mtu aaminiye huokolewa. Kila mtu aaminiye katika uponyaji huponywa. Baba, saidia kutokuamini kwetu sasa.

²³⁸ Umejitalambulisha Mwenyewe hapa usiku wa leo, kimaandiko, kutuonyesha sisi kwamba Wewe upo hapa. Sasa jalia itimie kwamba kila mtu anayepitia kwenye jukwaa hili, ama katika kusanyiko hili, jalia kusiwe na mtu dhaifu miongoni mwetu ibada itakapomalizika. Jalia Roho Mtakatifu mkuu aje miongoni mwa watu Wake na atutie upako, kila mmoja, Bwana, wahudumu hawa wote, hawa watumishi Wako wote wanaoketi hapa, mamia. Baba, ninaomba kwamba kila moja ya maombi yetu yatakuendea Wewe wakati tukiwa katika Uwepo wa Kiungu wa Utu Wako. Pia jalia watu hawa waelewe, wanapopita jukwaa hili, kwamba usiku wa leo ndio usiku wa uponyaji wao, kama wanaweza kuamini.

²³⁹ Sasa ninataka kila mtu aendelee katika maombi wakati watu wakipita, nami nitakuwa nikimwekea kila mmoja mikono kwa ajili ya uponyaji wao.

²⁴⁰ Njoo, bwana. Ninamwombea huyu, ndugu yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe.

²⁴¹ Ninamwombea huyu, ndugu yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe.

²⁴² Ninamwombea dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

²⁴³ Ninamwombea dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

Ninamwombea dada yangu, katika Jina la Yesu, kwa ajili ya uponyaji wake.

Ninamwombea dada yangu, katika Jina la Yesu, kwa ajili ya uponyaji wake.

²⁴⁴ Ninamwombea ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

²⁴⁵ Ninamwombea dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

²⁴⁶ Ninamwombea ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

Ninamwombea ndugu yangu, katika Jina la Yesu, kwamba Wewe utamponya.

²⁴⁷ Ninaweka mikono juu ya ndugu yetu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

²⁴⁸ Ninaweka mikono yangu juu ya ndugu huyu, katika Jina la Yesu, kwa ajili ya uponyaji wake.

²⁴⁹ Huku nimeweka mikono yangu juu ya ndugu huyu, ninaombea uponyaji wake, katika Jina la Yesu, wakati akiwa katika Uwepo wa Kiungo hapa sasa wa upako Wako.

²⁵⁰ Mponye huyu, dada yangu, Baba, ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo. [Dada huyo anasema, "Asante, Yesu."—Mh.]

²⁵¹ Baba wa Mbinguni, huku umati mkubwa wa watu ukiomba, tunatambua Uwepo Wako. Mponye dada huyu, ninaomba, katika Jina la Yesu.

Mponye dada yangu, Baba, katika Jina la Yesu, ninaomba.

Ninaweka mikono juu ya ndugu yangu katika ukumbusho wa Neno Lako, kwa ajili ya uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Jalia iwe hivyo, Baba, ishara hizi hufuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.

Jalia uponyaji wa ndugu yangu, Baba, ninapoweka mikono juu yake katika jina la Yesu Kristo.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya dada kwa ajili ya uponyaji wake.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya dada yangu kwa ajili ya uponyaji wake.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu kwa ajili ya uponyaji wake.

Ninambariki huyu, ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya imani ya uponyaji.

Bwana Yesu, ninaweka mikono yangu juu ya mtoto huyu, kwamba Wewe uponye mwili wake na umpe afya. Utafanya hivyo, Baba, Wewe uliahidi hilo.

Katika Jina la Yesu Kristo jalia dada yetu aponywe.

Jiwekee hiyo sasa, usitie shaka. Utakuwa mzima. Je! unaamini hilo? Unaamini hilo?

Katika Jina la Yesu, jalia dada yetu aponywe.

Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, jalia mtoto huyu aponywe. Usitie shaka. Amini.

Baba, mponye maskini dada huyu, ninaomba, katika Jina la Yesu. Amina. Usitie shaka. Sasa, je! mnaamini hilo? Mnaona, hivyo ndivyo inavyofanywa. Kile tu Yeye alichosema ufanye.

Baba, Mungu, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu katika jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Baba, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Baba, Mungu, huku mikono imewekwa juu ya ndugu yangu, ninaomba, katika Jina la Yesu, kwa ajili ya uponyaji wake.

Vile vile, juu ya ndugu yangu hapa, Baba, nimeweka mikono yangu, ukumbusho wa Neno Lako, na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba kwa ajili ya uponyaji wa ndugu yangu.

Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, ninaomba kwa ajili ya uponyaji wa dada yangu. Jalia iwe hivyo.

Bwana, ninaomba ya kwamba Wewe utamponya dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Dada Shirley. Mbona, ubarikiwe. Baba wa Mbinguni, ninaomba kwa ajili ya Dada yangu Shirley, kwamba Wewe utamponya, katika Jina la Yesu. Amina.

Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya dada huyu katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya uponyaji wake.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya dada yetu kwa ajili ya uponyaji wake.

Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya dada huyu. Ulisema tufanye hivyo, Bwana. Nami ninafanya hivyo kwa sababu kwamba ninakuamini Wewe. Ninajiunganisha mwenyewe, imani yangu, nafsi yangu pamoja naye, na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Amina.

Juu ya mvulana huyu mdogo, ninaweka mikono, katika Jina la Yesu, na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake.

Ninaweka mikono yangu juu ya dada huyu, katika Jina la Yesu, ninaombea uponyaji wake.

Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya dada, katika Jina la Yesu Kristo, ninaombea uponyaji wake.

Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya msichana huyu mdogo, katika Jina la Yesu Kristo, ninaombea uponyaji wake.

A-ha. Wewe na mtoto? Mtoto wako. Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya mvulana huyu mdogo na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Amina.

Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya msichana huyu mdogo, katika Jina la Yesu na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake.

Dada Waldrop, Mungu akubariki. Huyu hapa mama, hakika anajua maana ya uponyaji. Yeye alirudishwa kwenye uhai miaka kumi na mitano iliyopita katika mstari wa maombi, [Dada Waldrop anasema, “Ndiyo, ilikuwa miaka kumi na saba.”—Mh.] miaka kumi na saba iliyopita, alikufa kwa kansa moyoni mwake. Daktari ana rekodi yake hapa. Bibi Waldrop. Ni wangapi wanajua hiyo kuwa ni kweli, huko Phoenix, inueni mikono yenu?

Baba wa Mbinguni, uponyaji wako unadumu mradi tunaamini. Ninamwomba Dada Waldrop, mpe afya, katika Jina la Yesu. Amina. Akubariki, dada.

Baba wa Mbinguni, ninaomba uponyaji wa ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Baba, ninaweka mikono juu ya mvulana huyu mdogo, katika Jina la Yesu Kristo ninaomba uponyaji wake. Amina.

Baba, ninaweka mikono juu ya dada huyu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

Baba wa Mbinguni, ninaomba rehema na uponyaji kwa ajili ya dada yangu. Mjalie usiku wa leo. Ninaweka mikono yangu juu yake, kujiunganisha mwenyewe na maombi yangu kwa ajili ya uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Amina.

Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya dada yangu, nikiamini maombi yangu. Yeye anaamini, pia. Jalia aponywe, Baba, katika Jina la Yesu.

Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu, hapa, pia nikiamini maombi yetu, sote tukiomba pamoja, Baba, tunaamini kwamba hili litatendeka, ninaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Baba wa Mbinguni, huku nimeweka mikono juu ya dada huyu, ninaomba uponyaji wake katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Baba wa Mbinguni, tena, juu ya mwili wa maskini ndugu huyu anayesimama hapa, ninaweka mikono yangu, nikiamini kwamba Wewe unasikia, na maombi yangu pamoja na yake, pamoja na kanisa hili lote, tunaamini ya kwamba Wewe utamponya, katika Jina la Yesu. Akubariki, Ndugu.

Baba wa Mbinguni, ninaomba kwa ajili ya uponyaji wa dada yangu, huku mikono ikiwa juu yake, moyo wangu unawahurumia, Bwana. Mrehemu na umponye, katika Jina la Yesu.

Baba wa Mbinguni, maskini msichana huyu mzuri anapitia katikati ya kusanyiko, sawa na wazazi. Ninaweka mikono juu yake, katika Jina la Yesu Kristo, Yule aliyeweka mikono Yake juu ya watoto wadogo, kuwabariki. Jalia abarikiwe na kuponywa, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

Baba wa Mbinguni, nikiweka mikono juu ya dada yetu, anapopitia hapa, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Vivyo hivyo, juu ya dada huyu, Baba, ninaweka mikono, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu katika Jina la Yesu Kristo jalia aponywe.

Baba, Mungu, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

252 Vivyo hivyo, juu ya ndugu yangu hapa, Baba, ninaweka mikono yangu. Katika Jina la Yesu, jalia aponywe.

253 Baba, Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya dada yangu. Jalia aponywe, katika Jina la [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] Bwana Yesu. Samahani, Baba.

254 Ninaweka mikono juu ya ndugu huyu, na kuombea uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Amina.

255 Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu, na kuombea uponyaji wake, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

256 Baba yetu wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu, na ninaombea uponyaji wake. Nikiunganisha maombi yangu, Bwana, pamoja na maombi yake, na maombi ya kanisa ambao Wewe umawakusanya usiku wa leo. Mikono yangu juu yake, nikitambulisha imani yangu katika Mwana wa Mungu, ninaombea uponyaji wake. Amina.

257 Sasa tuna visa vya viti vya magurudumu hapa ninaotaka kuwaombea.

Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono yangu juu ya...?... rehemu na neema ziwe pamoja nao Bwana...?...katika Jina la Yesu Kristo. Vivyo hivyo, kwa maskini dada huyu, Bwana, Mungu. Shetani, tunakutoa kutoka kwao...?... Wajalie nguvu na maisha ya uvuvio; watie nguvu, Bwana...?...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

258 Yesu alisema, wakati mmoja, “Mnajua kile nilichowafanyia?” Nimefanya tu kile Mungu aliagiza kufanywa.

259 Sasa hebu na tuombe pamoja, kila mmoja. Unapoweka nia yako kwa Mungu, shikilia maombi yako. Kumbukeni, aminini sasa, aminini pamoja nasi. Kila mmoja wenu hapa, aliye mgonjwa, na labda hukuwa na kadi ya maombi...

²⁶⁰ Sasa, tutakuwa tukisambaza kadi za maombi tena, kesho usiku, saa kumi na mbili u nusu au saa moja, kitu kama hicho, saa kumi na mbili u nusu au saa moja, kwa hiyo tutakuwa na mstari wa maombi tena kesho usiku. Ninasikitika kwamba niliwachelewesha kidogo usiku wa leo, kwa sababu ya mstari wa maombi. Mungu na awabariki.

Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu tena.

²⁶¹ Tunapoomba, Baba, tunamsamehe kila mtu dhambi yake dhidi yetu. Kukipatikana chochote ndani yetu, kisicho cha jinsi Yako, tusamehe, Bwana. Kwa kuwa, tunaambiwa kwamba tunapaswa kuwa “nyaraka zilizoandikwa za Mungu, zinazosomwa na watu wote.” Na kama tulivyo zitii Amri Zako, tukauona Uwepo Wako ukijitambulisha Mwenyewe pamoja nasi; watu wamekuja kwenye jukwaa hili, wakishuhudia imani yao. Tumeweka mikono juu yao, Baba. Si tu kama mmoja wetu, bali sote pamoja, katika maombi, tumeweka mikono juu yao, tukiamini ya kwamba Wewe utaiponya miili yao.

²⁶² Wewe ulisema, wakati Wewe ulipokuwa hapa duniani, “mkiomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Yesu wa . . . Mwana wa Mungu, hiyo ilikuwa ni ahadi Yako, Bwana.

²⁶³ Na Yule aliyetoa ahadi amejitambulisha Mwenyewe hapa usiku wa leo kutimiza ahadi Yake. Kwa hiyo i—imetekelezwa, Amri Zako, kuweka mikono juu ya wagonjwa. Sasa, jalia itimizwe. Imeandikwa, jalia itekelezwe. Jalia nguvu za Yesu Kristo zitokeze usiku wa leo, na kumtenganisha kila mtu hapa ndani, kutoka kwa kutokuamini kokote, na jalia Uwepo wa Yesu Kristo, Neno, Yule anayejua mawazo ya moyo wetu, jalia Hilo lichukue mamlaka usiku wa leo katika kila moyo.

²⁶⁴ Pia tunamkemea Shetani na nguvu zake zote za giza, nguvu zake zote za kutokuamini. Roho wa Mungu ameinua kiwango dhidi yako, Shetani. Wewe ni kiumbe kilichoshindwa. Yesu Kristo alikushinda Kalvari.

²⁶⁵ Alifufuka, siku ya tatu, akashinda mauti, kuzimu, na kaburi. Alipaa Juu na kuwapa wanadamu karama. Yeye yupo hapa Mwenyewe usiku wa leo. Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Tunauona Uwepo Wake hapa usiku wa leo, ukitimiza Neno Lake. Kwa imani tunaamini kwamba kila mtu mgonjwa hapa ndani ataponywa, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo.

²⁶⁶ Nao watu wakasema, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mungu awabariki. Tunarudi kwa ndugu. 

NENO LA MUNGU LINAHITAJI UTENGANO
MKAMILIFU KUTOKANA NA KUTOKUAMINI SWA64-0121
(God's Word Calls For A Total Separation From Unbelief)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumanne jioni, tarehe 21 Januari, 1964, katika Hoteli ya Ramada kule Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org